Taarifa Rasmi ya Habari ya WRM 241

World Rainforest Movement

http://wrm.org.uy

WorldRainforestMovement / @WorldRainforest

Sauti toka Chini: Jamii katika Vuguvugu na Mikakati ya Upinzani

Mtazamo wetu: Jinsi ya Kuimarisha Mavuguvugu ya Upinzani?.....2

Brazili: Mimi ni Kum'tum, Ninatokea Jamii ya Watu wa Akroá-Gamela.....4

Wanakijiji nchini **Sierra Leone** wanatafakari juu ya hatma yao ya baadaye baada ya kushinda na kuipata tena ardhi yao toka kwa kampuni ya mafuta ya mawese.....8

Kuuhuisha Ustawi: Vijiji vya Kochi taluka, nchini **India**, wanapinga uchimbaji wa madini na wanafungua nafasi kwa ajili ya uongozi binafsi.....11

Upinzani wa Wanawake Walinzi wa Maeneo kwa Tasnia ya Uziduaji huko **Amerika ya Kusini**.....16

Tafakari kutoka **Afrika**: Ishinde hofu ya kujenga vuguvugu imara la mabadiliko.....21

Kuisimamia haki ya kusema HAPANA: Baraza la Kudumu la Watu wa **Afrika ya Kusini**.....25

Tanzania: Upinzani wa wanajamii dhidi ya mashamba makubwa ya miti.....28

*Taarifa Rasmi ya Habari ya WRM imedhamiriwa kuwa ni **nyenzo ya kusaidia na kuunga mkono mapambano ya wanajamii wanaolinda ardhi na misitu yao.** Pia taarifa hii imedhamiriwa **kuzifanya sauti za mapambano mengi ya upinzani kusikika na kufahamika**, Hivyo, katika kila toleo, tunajaribu kuwaalika watu na makundi tofauti kuchangia makala zao au kutoa taarifa zao nyingine ambazo ni muhimu. Zaidi ya yote, taarifa hii inalenga kuwa ni **nyenzo ya kuwafahamisha** watu wanaotegemea misitu kuhusu mipango na juhudi za kimataifa zinazohusu misitu **na kuwaonya** juu ya uwezekano wa hatari na athari zinazoweza kuwakuta katika maisha yao.*

Taarifa rasmi ya habari ya WRM inatawanywa kwa barua-pepe, na kupitia mitandao ya kijamii kama vile Facebook na twitter na pia unaweza kuisoma taarifa hii katika tovuti ya WRM. Kama hadi sasa hupokei taarifa hii, unaweza kujiunga na kupata taarifa hii bure katika tovuti ya WRM (http://wrm.org.uy). Ikiwa utapenda kuchangia wazo au makala au ikiwa utapenda kuangazia mapambano katika ngazi ya kimataifa, basi tunaomba uandike barua pepe kwenda wrm@wrm.org.uy

Mtazamo Wetu
Jinsi ya Kuimarisha Mavuguvugu ya Upinzani?

Ni ukweli usiopingika kuwa misitu ya asili inaharibiwa sana kwa kiwango cha kasi sana. Ekari nyingi sana maelfu kwa maelfu zinaharibiwa ili kupisha miradi ya uchimbaji wa madini, uziduaji wa mafuta na gesi asilia, upandaji wa miti kama vile Mikaratusi au michikichi ya mafuta ya mawese, mabwawa ya kuzalishia umeme, utoaji wa vibali vya kukata magogo, na miradi mikubwa ya ujenzi wa miundo mbinu, na mambo mengine mengi.

Lakini pamoja na madhara mengi ambayo hakuna anayeweza kukana yanayotokana na shughuli hizi ulimwenguni kote, shughuli hizi pia zinasababisha ujio wa mambo mengine kujitokeza: na baadhi ya mambo yanayojitokeza ni pamoja na **mavuguvugu mbalimbali yaliyo imara kutoka kwa wanajamii walioathiriwa wanaoyalinda maeneo yao, njia zao za kimaisha, tamaduni na imani zao, na hata uwepo wao.**

Pamoja na ukandamizaji mkubwa wa kuwabambikizia watu kesi za jinai na vurugu mbalimbali toka kwa baadhi ya makampuni, pamoja na serikali za sasa kuruhusu vitendo hivi viovu kuendelea, pamoja na mawakala wa “maendeleo” na taasisi za fedha kuendelea kutoa fedha na kuunga mkono biashara hizo ili ziweze kuendelea; ukweli ni kuwa wanajamii na watu wengi hawajaacha kujikusanya, kujipanga, kuratibu na kupinga mauaji kwa jina la mfumo wa “maendeleo.” Pasipo mapambano haya, ni hakika kuwa misitu, vyanzo vya maji na maeneo mengine yataharibiwa kwa ukubwa zaidi.

Taarifa hii rasmi ya habari ni tafakari kuhusu mavuguvugu mbalimbali ya upinzani na changamoto kubwa sana zilizopo leo hii, na kuhusu changamoto zile zitakazokuja baadaye. **Tunajiuliza: ni jinsi gani mavuguvugu haya ya upinzani na mashirika mengine katika ngazi ya jamii yanavyoweza kuimarishwa kwa lengo la kuzuia uharibifu wa misitu na watu katika muktadha wa sasa duniani?**

Mahojiano na Kum’Tum wa jamii ya watu wa Akroá-Gamela, katika lango kuingilia kwenda misitu ya **Amazon ya Brazili**, yalitufikisha katika mchakato binafsi na wa pamoja ambapo suala la **kuzirejelea kumbukumbu na kupaza sauti kama watu yalikuwa ni mambo makuu katika kujiunganisha na kudai ardhi na uhai.** Kum’Tum anatukumbusha kuwa, "**Hatudai ardhi kwa ajili ya uzalishaji tu. Tunaidai ardhi kwa kuwa ni mahali patakatifu; ni mahali panapotoa maana ya uwepo wetu.**”

Kutoka **Sierra Leone** tunapata hadithi ya wanajamii wa Port Loko, ambao—baada ya takribani miaka kumi ya mapambano dhidi ya kampuni iliyokuwa imenyakua ardhi yao kwa njia za ulaghai na kisha ikaijaza ardhi hiyo kwa michikichi ya mafuta ya mawese—**hatimaye mahakama imeamua ardhi hiyo irudishwe kwa wanajamii.** Ni dhahiri kuwa mchakato wa uratibu kati ya mashirika ya wanajamii katika ngazi ya chini, katika kanda, na katika ngazi ya

kimataifa unaonekana kuwa ni wa muhimu sana katika mapambano hayo. Kwa sasa wanajaribu kufikiria jinsi watakavyoitumia ardhi yao kubwa ambayo imegubikwa na mistari mingi ya michikichi ya mafuta ya mawese.

Kutoka **India**, kuna makala inayoangazia aina mbalimbali za kuyahuisha na kuyajenga upya mashirika ya kwenye ngazi za jamii katika mji wa Korchi, Mahrashtra. Kwa kutoa mkazo maalum juu ya wanawake kuungana, makala hii inaeleza jinsi **walivyofanya sauti zao zikasikika—sio tu kwa lengo la kupinga uchimbaji madini bali pia kupinga aina mpya za ufanyaji maamuzi katika ngazi ya kijiji na ngazi za juu za kijiji.** Baadhi ya vitendo wanavyovifanya ni kuwa vikundi hivi vingi vinatengeneza mikakati ya kuhifadhi misitu kwa usimamizi wao katika ngazi ya chini, wanaufufua utambulisho wao wa kiutamaduni, wanaikiri na kuithibitisha demokrasia ya moja kwa moja na demokrasia ya kijinsia na wanahoji juu ya mifumo ya sasa ya maendeleo.

Kutoka **Amerika ya Kusini**, kuna makala nyingine inayoangazia juu ya **mashambulizi mengi kwa wanawake wanaolinda na kutetea maeneo**. Makala hii inaelezea jinsi wanawake wanavyoweza kufanya matendo mbalimbali ambayo yamewawezesha kuisimamia na kuiweka hadharani mitazamo yao mbalimbali tena ya kipekee, na jinsi ambavyo kwa nyakati nyingi wameweza kuzuia au kusimamisha kwa muda shughuli za uziduaji. Wao wanakazia juu ya **mchakato wa uponyaji kuwa ni jambo la msingi katika mjadala wa ufahamu kati ya watu, muktadha, na vizazi —na kutokea mahala pa uthibitisho wa kumbukumbu za wanawake wahenga.**

Taarifa hii rasmi ya habari pia imejumuisha **mahojiano na mwanaharakati wa Kikameruni na mtetezi wa haki za binadamu, Nasako Besingi.** Besingi anatukaribisha kutafakari juu ya ukweli kuwa katika sheria nyingi za nchi za Kiafrika, ardhi "ni mali ya Serikali." **Pia anatuonyesha mikakati muhimu na changamoto zilizopo katika kujenga vuguvugu imara la mabadiliko.** Nasako Besingi anasema, “Ili vuguvugu la upinzani liweze kufanikiwa —ni muhimu sana kuimarisha mshikamano wa wananchi na kupata safari za mafunzo za kubadilishana uzoefu kati ya vijiji ambavyo vimeathiriwa moja kwa moja na vile ambavyo havijaathiriwa moja kwa moja na miradi mbalimbali ya uwekezaji—ili kuwajengea wananchi ujasiri katika ngazi za wananchi."

Kutoka **Afrika Kusini**, kuna makala inayotueleza juu ya **Baraza la Kudumu la Watu**, ambapo zaidi ya kesi ishirini toka katika eneo hilo ziliweza kuwasilishwa na kusikilizwa. Baraza limekuwa **ni Jukwaa muhimu sana kwa wanajamii kuweza kuelezea mapambano yao na katika kujenga mshikamano.** Kesi ya wananchi wa Xolobeni nchini Afrika ya Kusini imekuwa ni ishara bora. Mwezi Novemba 2018, baada ya miaka 16 ya mapambano dhidi ya kampuni kubwa ya uchimbaji wa madini ya Australia, mahakama iliamua kwa kuwapendelea wananchi; mahakama ikasema kuwa kabla ya kutoa kibali cha kumiliki na kuchimba madini ni lazima ridhaa “kamili na rasmi” itolewe na mji wa Xolobeni.

Makala nyingine inaelezea juu ya habari ya kampuni ya upandaji miti inayoitwa **Green Resources nchini Tanzania.** Makala hii inatuonyesha kuwa mara zote makampuni haya yanahitaji kupata eneo kubwa la ardhi, na ili yaweze kufanya hivyo, wao hutoa orodha ya ahadi nyingi ambazo mara nyingi huwa hazitekelezwi kwa lengo la kuwashawishi wanajamii ili waweze kuitoa ardhi yao. Hata hivyo, wananchi wa kijiji cha Nzivi walijifunza na kupata uzoefu kwa wakati na hivyo wakaamua kusema hapana kwa kampuni yoyote inayotaka kumiliki kiwango kikubwa cha ardhi yao. Makala hii inaonyesha **umuhimu wa kupashana habari na hadithi mbalimbali kati ya wananchi wanaokabiliana na hali zinazo shabihiana.**

Mapambano Bado Yanaendelea!

Brazili: Mimi ni Kum'tum, Ninatokea Jamii ya Watu wa Akroá-Gamela

Kwa mujibu wa ramani na taarifa za karne ya 18, watu wa jamii ya Gamela, kama walivyoitwa na Wareno waliishi katika eneo linaloitwa Maranhão katika mkoa wa Baixo Pindaré —sehemu inayohusisha manispaa za Codó, Monção, Cajari, Viana na Penalva. Bibi yangu alizaliwa na kukulia katika kijiji cha Capibari kilichopo Penalva; na mama yangu alizaliwa manispaa ya Monção, katika eneo linaloitwa Jacareí, na hapo ndipo mahali nilipozaliwa na mimi. Ni eneo kubwa ambalo lilikuwa likimilikiwa na bado linakaliwa na watu wa jamii ya Akroá-Gamela.

Hivi nilivyo ni matokeo ya mchakato huu wa vurugu na ukoloni. Wakati angali bado kijana, bibi yangu alichukuliwa toka kijijini kwao na familia ya wazungu waliokuwa wakiishi mjini. Mama yangu alizaliwa mbali na kijiji chetu. Mimi pia nilizaliwa mbali na kijiji chetu. Kwa kuwa **alama za ukoo zipo katika mwili, na pia zipo—hasasaha —katika nafsi,** basi uliwadia wakati ambapo nilianza kujiuliza juu ya alama hizi nilizozibeba. Ni kutokana na mchakato huu wa kuutafuta ukweli, mchakato ambao ninapenda kuuita kuzirejea fikra, ndipo nikaamua kuitafuta mizizi ya ukoo ili niweze kuelewa sawasawa juu ya alama nilizonazo katika mwili na katika nafsi yangu. Lakini jambo hili ninalolifanya si langu binafsi, bali ninalifanya kwa ajili ya jamii yangu kwa pamoja. **Kwa sasa tunagundua kuwa sisi hatupo peke yetu hapa ulimwenguni, na kwamba alama hizi si alama za mtu binafsi; bali ni alama za watu, zinazofanana na zenye mizizi yenye kina kirefu.**

Kwa muda mrefu, bibi yangu na mama yangu waliutumia ukimya kama mbinu ya mkakati wao. Katika mazingira ambapo Serikali ilikuwa imejikita katika kukanusha mambo mengi, basi uamuzi ulikuwa ni kunyamaza kimya. Nilichojifunza leo ni kwamba ukimya ni aina mojawapo ya upinzani. Ni kipindi ambacho tunapaswa kuwa kimya ili tuweze kuendelea kuwepo. Hivyo, ni kinyume na yale ambayo watu wanayasikia, ukimya haumaanishi ni kuidhinisha vurugu zinazofanywa na Serikali. Kwa upande wa watu wetu wa makabila ya kiasili, ukimya ilikuwa ni —kwa ujumla wake—mkakati wa upinzani. **Ili kuwa na uelewa na hisia zinazofahamu kuwa ni kwa nini watu fulani wanafanya jambo moja au jingine, basi ni dhahiri kuwa jambo hilo linawezekana pale tu mtu anapozifanyia uchambuzi kumbukumbu za pamoja za watu hao.**

Kwa sasa babu zetu wanasema kuwa tupo katika eneo linaloitwa Taquaritiua, eneo ambalo watu wa makabila ya kiasili waliweza kwenda na kuishi. Watu wa makabila ya asili waliweza kufika mahali hapo toka katika misitu ya mvua, hasa kuanzia mwezi wa Agosti. Utaratibu huo uliingiliwa na kuvurugwa. Paliwekwa mkongo wa simu ambao ulianza kuligawa eneo lao. Na hadi kufikia miaka ya 1960 kulijitokeza mchakato uliojaa vurugu wa uporaji wa ardhi uliofahamika kama "grillaje", mchakato huu uligubikwa na nyaraka na vielelezo vilivyo jaa uongo na udanganyifu. **Lengo kuu la vurugu hizi zote ilikuwa ni kukanusha kuwa koo za**

makabila hayo ya kiasili ziliishi katika ardhi hiyo hapo kabla. Uwepo wetu kama binadamu ulikanushwa pia.

Ukanushaji huo ulianza kutengeneza utengano. Watu walitengwa mbali na ardhi yao kikamilifu kwa kuzingatia: watu, misitu, maji, mito, na maeneo matakatifu. Wakati uzio ulipoanza kujengwa, basi watu nao wakaanza kutengana na kupotezana; na kwa sababu hiyo mipaka ikawekwa katikati ya watu na hivyo kuwatenganisha. Kwa sababu hiyo hata mahusiano kati ya watu yaliingiliwa na kuvurugwa. Tunapochukua hatua za kuokoa na kujiunganisha na kumbukumbu za koo zetu kwa pamoja, basi jambo hilo linawezekana ikiwa tu tutajiunganisha na yale maeneo ambayo ndiyo yanayotoa maana na historia ya uwepo wetu. Mambo haya mawili ni muhimu na yana uhusiano wa karibu sana. **Kuyarejea maeneo ya ardhi yetu—ikiwemo hata yale ambayo bado yamewekewa uzio—ni muhimu sana kwa kuwa yanaleta maana ya uwepo wetu kama watu.** Hivyo kuna umuhimu wa kufanya kazi ya kuzifanyia tathmini kumbukumbu zetu. Ni mchakato ambao unatokea katika moyo. Ikiwa mchakato huo unatokea katika moyo, basi ni kitu kinachowezekana kukiamsha au kukitupilia mbali.

Historia, Eneo na Kuidai Ardhi

Kuna nyaraka zilizojitokeza kuhusu eneo la [ardhi] lilitolewa kama mchango [kwa watu] wakati wa kipindi cha ukoloni mwaka 1759; jambo ambalo linaleta mkanganyiko maana linaonyesha tulipewa kitu ambacho tayari kilikuwa ni mali yetu. Sasa ninaongelea maalum kabisa kuhusu mojawapo ya ardhi hizo: yaani ardhi ya eneo la Taquaritiua ambayo ipo katika manispaa ya Viana. Nyaraka hizo za mwaka 1759 zinaongelea eneo la hekta elfu 14 au elfu 15. Na zilikuwa nyaraka zenye ulinzi mkali.

Mwaka 1969, Sheria ya Ardhi ya Sarney (1) iliifanya ardhi ya umma kuwa huru kwa ajili ya kutwaliwa, na hadi kufikia mwaka 1970s, eneo la Maranhão lilikabiliwa na mchakato uliojaa vurugu uliojulikana kama "grillage" (Yaani: Uporaji wa Ardhi). Katika miaka ya 1970 na 1980, tuliishi chini ya mchakato ambapo lile eneo lililotolewa kama mchango mwaka 1759 liligawanywa na kuwekewa uzio. Matokeo yake ni kuwa hivi sasa 2018, ardhi yote inayotajwa katika nyaraka hizo za tokea karne ya 18 imesajiliwa kwa majina ya watu binafsi katika usajili wa manispaa ya Viana.

Lakini ilipofikia mwishoni mwa miaka ya 1990, vuguvugu la ndani lililojulikana kama *"rumo"* lilianza katika maeneo yaliyokuwa yameporwa kwa lengo la kujikimu kimaisha. *"Rumo"* ni pale familia inapokwenda kufanya kazi katika kipande cha [ardhi] katika maeneo ambayo yamekwisha sajiliwa kwa majina ya watu wengine. Ni mchakato wa kizamani wa kudai na kuipata ardhi. Kulikuwa na msukumo mkubwa wa kutaka kuziondoa hizo familia zilizokuwa zikidai ardhi yao kwa nguvu. Hatimaye maamuzi yalifanyika: “Hapana, kuanzia sasa na kuendelea, wavamizi hawataweza kuweka tena vizuizi; kugawa na kuweka mipaka ya vitalu vya ardhi.” Kwa hakika ulikuwa ni upinzani muhimu sana kwa ajili ya uendelevu wa watu, ingawa ilikuwa ni katika eneo dogo la ardhi. Familia nyingine ziliondolewa na hivyo zikaamua kwenda mjini; watu wakatawanyika. **Lakini hivi karibuni mchakato wa kudai ardhi umewezekana kwa kuwa kulikuwa na nguvu kubwa iliyosaidia vuguvugu hili.**

Mwaka 2015 tuliamua kudai baadhi ya vipande vya ardhi, hasa vipande vya ardhi vilivyokuwa karibu sana na nyumba za makazi kwa lengo la kupata eneo la kulima. Lakini kuna jambo moja katika mchakato huu wa kuipata ardhi ambalo ni la muhimu sana kwetu, ni lile la kuwa na kumbukumbu za eneo: yaani kudai maeneo matakatifu. **Hatudai ardhi kwa ajili ya uzalishaji tu. Tunaidai ardhi kwa kuwa ni mahali patakatifu; ni mahali panapotoa maana ya uwepo wetu.**

Hivyo ilikuwa ni muhimu sana tulipoamua kujipanga tena na kuuelezea ulimwengu kuwa sisi tunaishi kama watu. Na hili ndo nililokuwa nikilisema pale mwanzo: kuna wakati wa kukaa

kimya ili muweze kuishi na kuwepo, na pia kuna wakati wa kuongea ili muweze kuishi na kuendelea kuwepo. Tupo katika wakati ambao ni muhimu sana—na uliokuwa muhimu sana na utakaoendelea kuwa muhimu sana—yaani tuongee ili tuweze kuendelea kuwepo na kuishi.

Mpangilio, Chuki na Vurugu

Tangu mwanzo, tulitaka mpangilio wetu uwe wa kufanya kazi kwa pamoja. Hatukuwa na mtu aliyekuwa ndiye msemaji mkuu: sauti ilipaswa kuwa ya wanajamii wote. **Tulipaswa kuanzisha mchakato unaoendelea wa majadiliano miongoni mwetu ili tuweze kufanya maamuzi.** Ilikuwa ni mchakato wa kudumu wa kukutana, ili kujenga makubaliano miongoni mwetu; na pia, mchakato ulijengwa katika namna ambayo wazee walitueleza jinsi tulivyokuwa tunajipanga—jambo ambalo kwa wakati fulani lilinyamazishwa ili kutufanya tuendelee kuwepo na kuishi. Lakini jambo hilo halikuwa limepotezwa, na tunaendelea kusema “utaratibu huu umekuwa ndio njia yetu au namna yetu ya kufanya mambo."

Mwaka 2014 tulianza kupata vitisho kutokana na kujipanga kwetu kama watu kwa umoja wetu. Mwaka ule, kampuni ya nishati ya Maranhão, inayoitwa Cemar, ilianza kujenga msongo wa kusafirishia umeme. Tuliwaomba wasimamishe ujenzi ili waweze kukamilisha taratibu na mawakala wa mazingira. Kampuni ya Cemar ilidai kuwa "wanaojiita makabila ya asili" wanazuia maendeleo ya mkoa. Ni dhahiri kuwa watu wengi wanaopinga mradi huu hawawezi kunufaika na hayo maendeleo wanayoyasema; lakini cha ajabu wanaendelea kusema kuwa sisi tunayapinga hayo maendeleo.

Mwezi Aprili 2017, katika majadiliano na radio moja ya wananchi, makamu wa shirikisho anayeitwa Aluísio Mendes alitutaja sisi "tunaojiita makabila ya kiasili,” kuwa ni waandamanaji na wavamizi, na akasema kuwa sisi tunawapora watu wenye nidhamu na watulivu. Waliandaa utaratibu wa "matendo ya amani," lakini kwa sasa tunafahamu kuwa tangu mwanzo, hilo lilikuwa ni tendo la kujiandaa na kulivamia vuguvugu letu la kudai ardhi. Waliendelea na nia yao na wakatuvamia. (2) Ushiriki wa viongozi wa kanisa la Assemblies of God *(Kwa Kiswahili: Kusanyiko la Mungu)* katika mchakato huu ni jambo jingine muhimu sana. Wao ndio waliokuwa wakisimamia na kupanga mikakati ya upinzani katika mkoa,—na zaidi ya kuandaa na kupanga—walikuwa wakiueneza ujumbe [kuhusu] "wavamizi wanaotishia amani na utulivu." Mambo haya yote yalitoa msingi wa uvamizi. Katika vipindi vya redio watu walieleza kuwa “mashambulizi” tuliyokuwa tukiyafanya yalikuwa yamesababisha baadhi ya watu wazee kufariki na kwamba baadhi ya wanawake mimba zao zilitoka. Maneno hayo yalikuwa ni kama baruti na moto uliowafanya watuvamie. Jambo la kushangaza kabisa, walianza kutulaumu kwa vifo vya watu ambao walikwa hawahusiki na mgogoro na hali iliyokuwepo. Mazingira ya ulipizaji kisasi na chuki yalitengenezwa dhidi yetu.

Jamii Zilizojipanga

Katika Mfumo wa Watu wa Kiasili na Wanajamii wa Maranhão, tayari tunayo makundi mengine ya kiasili kama vile quilombolas, wakazi wa pembezoni mwa mito, makundi ya wavuvi, wakataji wa nazi na wakulima, makundi haya yote yameweza kuwepo kwa uwezeshaji wa vitengo vya serikali. Mfumo huu ulianza mwaka 2011, wakati ambapo vuguvugu linaloitwa Moquibom quilombola lilipoivamia taasisi inayojulikana kwa kifupi kama INCRA (National Institute of Colonization and Agrarian Reform), na hii ilitokana na uwepo kwa vurugu kufuatia kiasi cha wanajamii zaidi ya 400 walipowasilisha madai yao mbele ya shirika hili—huku kukiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa (3).

Tarehe 30 Oktoba 2010, kiongozi mmoja wa jamii ya quilombola aliyeitwa Flaviano na aliyekuwa akitokea eneo la Charco aliuawa. Mwendesha Mashtaka wa serikali alitoa maelezo yanayopinga kuhusika kwa wamiliki wa ardhi, wasaidizi wao na walinzi waliokuwa na silaha. Sisi tuliliona jambo hili kuwa ni ujumbe wa wazi kabisa kwa watu wote waliokuwa

wakihusika na vuguvugu la quilombola. Mwezi Juni, watu walipiga kambi mbele ya Mahakama Kuu ya Serikali ya Maranhão kwa kuwa ilitolewa amri ya kuwafikisha wamiliki wa ardhi mahakamani kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Flaviano. Baadaye kambi za wananchi zilihamia kwenye makao ya INCRA, kwa kuwa tulifahamu kuwa kitendo cha kupooza kwa mchakato wa uwekaji mipaka ya ardhi ya quilombola kulisababisha vurugu na matishio ya vifo.

Mwaka huo huo, zaidi ya viongozi sabini wa Maranhão walipokea vitisho vya kuuawa. **Ilikuwa ni vigumu kutatua shida ya vitisho na vurugu nyingine pasipo kwanza kutatua mgogoro wa ardhi.** Hali hiyo ya sintofahamu ilidumu kwa siku kumi na mbili. Tulijikuta tupo pamoja, yaani watu wa quilombola na sisi watu wa jamii za kiasili na watu wa kiasilia na watu wa quilombola; na tukaona kuwa tulikuwa na matatizo yanayofanana: **yaani mapambano kwa ajili ya kupata eneo na ardhi yetu kwa mujibu wa fikra za mahali petu tulipotoka.** Baadaye kidogo tulifanya juhudi za kumiliki kwa kuweka kambi kwenye majengo maalum, na ilipofikia mwezi Novemba 2013 tulikuwa na kusanyiko jingine katika eneo la Santa Helena, ambapo watu sabini toka watu wa Maranhão na wanajamii wengi wa quilombola walikusanyika. Ndipo tukasema, "tunahitaji kurasimisha muungano na umoja wa pamoja." Ilikuwa ni jambo jema sana, maana tulitumia alama inayo onyesha kuwa fimbo moja ni rahisi kuivunja ilhali fimbo zikiwa nyingi ni vigumu sana kuzivunja. Na hiyo ikabakia kuwa ni alama na ishara ya nia yetu yakuendelea kuungana katika mapambano ya kuipata tena ardhi na maeneo yetu.

Tunahitaji maeneo yetu yaliyo huru. Kwa sababu hii, tunahitaji kuiweka ardhi iwe huru kwa kuondoa vizuizi na uzio uliokuwa umezungushiwa katika ardhi. Lakini kulikuwa na vizuizi vingine vilivyokuwa vikiizuia na kuifunga miili yetu. **Tuliamua kuiweka huru ardhi na kuiweka huru miili yetu. Tunautazama mwili kuwa ni kama kifundo cha uhusiano kati yetu na ardhi, maji, mimea, na wadudu.** Katika maeneo mengine jambo hili lingehusisha mchakato wa kuuondoa ukoloni. Wakati watu wanapoipata nguvu itokanayo na uwepo wa ardhi yao, basi nguvu hiyo itaifikia mioyo yao na kuwaweka huru.

Mfungamano wetu ni huu mradi wa muungano na umoja miongoni mwetu tunaoendeleza mapambano. Mtazamo wetu hauangalii kile ambacho watu wengine watatufanyia sisi. **Kwa hakika si shirika au muungano wa mashirika; na wala si Serikali. Bali ni sisi wenyewe. Ni lazima jambo hili litoke ndani yetu. Na tena, kuzingatia mambo ya msingi ya kumbukumbu ni muhimu sana.** Tunapovunja na kukata kata vizuizi na uzio wa waya, tunafanya hivyo kwa sababu vitu hivyo havikuwepo pale hapo kabla; bali kuna siku ndo viliwekwa. **Tunapozungumzia kuvunjavunja uzio uliopo ndani yetu, hapo tunazungumzia kuvunja chuki, ubaguzi, vurugu, na mfumo dume.** Kutokana na uwezo wetu wa kuweza kujiunganisha na nguvu inayotoka katika ardhi, basi ni lazima tuyaendeleze mapambano yetu.

Na hakuna nafasi ya wazo la mtu mmoja mmoja kumiliki ardhi—iwe ni ardhi kubwa, ya kati, au ndogo, au ndogo zaidi. Mtu hawezi kugawa kundi la mti wa mchikichi *(juçaral)* vipande vipande (4). Kundi la miti ya mchikichi ni mahali ambapo watu wote wanaweza kwenda kutafuta na kupata chakula. **Kimsingi, kuigawa ardhi katika vipande vipande kunaruhusu kuzalisha fikra duni inayofikiria kuwa ardhi ni kama kitu ambacho baadaye unaweza kukiuza. Ardhi si mali yetu. Sisi wanadamu ni mali ya ardhi na dunia.** Uwepo wetu unaleta maana kutokana na uhusiano wetu na ardhi.

Hebu tuzungumzie kuhusu mbinu ya Mfumo: Bila shaka si rahisi kuweza kufanya mkutano na meza ili kujadili mambo mbalimbali hata kama meza hiyo ingekuwa ya thamani kiasi gani. Meza inapaswa kuwa ni mahali ambapo watu wanaweza kuongea. Muda wa mazungumzo ni muda ambao kila mtu anahitaji kuongelea kuhusu mapito na uzoefu wake na uwepo wao. Kucheza, kuimba, kupiga ngoma, na kucheza maracas—yote hayo ni sehemu tu ya mambo yatakayounda mazungumzo. Mambo hayo si vitu, bali ni sehemu ya mazungumzo muhimu.

Ikiwa hatuna ukoo wowote ule, basi ni hakika kuwa mapambano yetu yote yataishia kuwa vurugu. Serikali ambayo haiheshimu misingi ya hizi koo ni serikali yenye vurugu na maasi — haijalishi kuwa serikali hiyo ni ya mlengo wa kulia au kushoto. Kanuni hii pia ni muhimu sana kwa vuguvugu lolote lile la mabadiliko bila kujalisha nia yake nzuri: ikiwa vuguvugu la mabadiliko halina msingi katika koo, basi ni hakika vuguvugu hilo litaleta vurugu, kwa kuwa litasababisha fikra ya kuwatenga na kuwakana wengine, na kuwasema kuwa ni wa aina nyingine.

(1) Sheria Nao. 2979 tangu Juni 15, 1969 iliweka na kuifanya ardhi ya umma iweze kuuzwa na ikasababisha uporaji wa ardhi na migogoro ya wakulima. Sheria hii imepewa jina la José Sarney, mmoja kati ya wajumbe wakuu wa serikali wa Maranhão, aliyekuwa gavana wa jimbo wakati huo na baadaye akawa raisi wa Brazili kati ya Aprili 1985 na Machi 1990.
(2) Tarehe 30 Aprili 2017 zaidi ya watu 30 wa makabila ya kiasili walikabiliwa na vurugu kubwa sana kiasi cha kuwaacha watu watano wakiwa wamejeruhiwa kwa risasi (Kum'tum akiwa ni mmoja wao), watu wawili kati yao walipata ulemavu wa mikono (mmoja wao alikatwa kichwa) na wengine kumi na tano walijeruhiwa, wakiwemo vijana wadogo. Kwa taarifa zaidi, tazama hapa: https://www.campoemguerra-reporterbrasil.org/eles-sao-mesmo-indios-a-pergunta-po
(3) Jamii ya Quilombola imeundwa kutokana na koo za watu wa Afrika waliolazimishwa utumwani na serikali ya kibepari ya Brazili. Moquibom ni moja kati ya mashirika ya watu wa jamii ya quilombola wa jimbo la Maranhão, jimbo ambalo ndilo lenye idadi kubwa ya watu wa jamii hii. INCRA ni wakala mwenye dhamana ya kusajili ardhi ya watu wa jamii ya quilombola.
(4) Neno *juçaral* lina maanisha ni kundi la miti ya michikichi inayotoa chakula kwa ajili ya wanajamii.

Wanakijiji nchini Sierra Leone wanatafakari juu ya hatma yao ya baadaye baada ya kushinda na kuipata tena ardhi yao toka kwa kampuni ya mafuta ya mawese

Ph: Grain.

Wanakijiji katika Wilaya ya Port Loko, nchini Sierra Leone wanashangilia. **Hii ni baada ya mapambano ya zaidi ya mwongo mmoja dhidi ya kampuni iliyokuwa imepora ardhi yao na kisha kupanda michikichi ya kuzalisha mafuta ya mawese, mahakama imeamua na kuridhia kuwa ardhi hiyo ni lazima irudishwe kwa wananchi.** Kwa sasa wanajaribu kufikiria jinsi watakavyoitumia ardhi yao kubwa ambayo imegubikwa na mistari mingi ya michikichi ya mafuta ya mawese.

Sakata hili la wanakijiji wa Port Loko lilianza mwaka 2009, wakati mwanajeshi wa zamani wa kikosi maalum cha Kiingereza alipokwenda Sierra Leone ili kuchukua ardhi kwa ajili ya upandaji wa michikichi ya mafuta ya mawese kwa niaba ya kampuni ya Uingereza yenye kificho na ambayo haikuwa na uzoefu kwenye biashara ya mazao ya kilimo. Ndani ya kipindi

cha miaka mitatu, Ndugu Kevin Godlington alipata mikataba ya kumiliki zaidi ya hekta 200,000 za ardhi katika wilaya za Pujehun, Tonkolili na Port Loko. (1) Mara baada ya hapo, mikataba mingi ya ardhi kati ya hiyo iliuzwa kwa mamilioni ya dola kwa makampuni mengine ambayo yalianza kufanya kazi ya kusafisha hizo ardhi na kisha kupanda mashamba makubwa ya michikichi ya mafuta ya mawese. Mkataba wa ardhi katika wilaya ya Port Loko uliuzwa kwa kampuni ya Siva Group, ambayo ni kampuni yenye makao yake nchini Singapore na inayomilikiwa na mfanya biashara bilionea wa Kihindi. (2)

Mikataba aliyoifanya Ndugu Godlington iliandaliwa na kutengenezwa huku ikikiuka misingi na taratibu nyingi za kimataifa zinazohusu ridhaa ya wananchi. **Katika mazingira mengi, viongozi wa wananchi walifikiria kuwa wanasaini risiti za zawadi za Krismasi ingawa kiuhalisia walikuwa wanasaini nyaraka zinazoridhia kuitoa ardhi yao kwa hao wageni.** (3)

Kijiji cha Mamanka kilichopo katika mamlaka ya Chifu wa Bureh, Wilaya ya Port Loko, ni moja kati ya wananchi waliokuwa wamepoteza ardhi yao kupitia mchakato huu. Mwaka 2009, kampuni ya Godlington iliyokuwa inaitwa Kampuni ya Kilimo ya Siera Leone (Sierra Leone Agriculture Ltd), ilisaini mikataba ya ardhi iliyoipatia kampuni hiyo hekta 6,557 za ardhi yao, huku ikiwaacha wanajamii wakiwa hawana ardhi ya kutosha kwa uzalishaji wa chakula. Mkataba huo ulikuwa ni sehemu ya mkataba mkubwa wa hekta 41,582 uliokuwa ukihusisha vijiji vingine kadhaa katika wilaya hiyo. Baada ya mwaka mmoja, kampuni ya Siva Group ilizinunua hisa za kampuni yenye jina la Kampuni ya Kilimo ya Sierra Leone (Sierra Leone Agriculture Ltd) kwa asilimia 95% huku Ndugu Godlington akibakiza hisa zake kwa asilimia 5%. (4)

Mwezi Agosti 2018, wawakilishi wa mashirika ya GRAIN, WRM na Bread for All tuliongozana na viongozi wa wanajamii katika maeneo yaliyo athiriwa na mashamba ya michikichi ya mawese katika nchi za Africa ya Magharibi na Kati ili kwenda katika kijiji cha Mamanka ikiwa ni sehemu ya warsha (5) iliyokuwa imeandaliwa na mashirika ya Sierra Leone Network on the Right to Food (SiLNoRF) – *(Kwa Kiswahili: Mtandao wa Haki ya Chakula wa Sierra Leone)*– , na Women's Action for Human Dignity (WAHD) – *(Jitihada za Wanawake kwa Ajiil ya Heshima ya Mwanadamu)*.

Tulienda kwa hao wanakijiji tukiwa na nakala ya mkataba wa ardhi ambao ulikuwa umesainiwa na kampuni ya Sierra Leone Agriculture Ltd. (6) Tulishangaa sana, maana hii ndio ilikuwa mara ya kwanza kwa wanakijiji kuiona nakala ya mkataba. Wanakijiji waliopoiangalia ile nakala ya mkataba waligundua mara moja kuwa ilikuwa imejaa ulaghai na udanganyifu. Wananchi walitueleza **kuwa hakuna hata kiongozi mmoja toka katika jamii yao aliyekuwa ameusaini mkataba ule, na kwamba baadhi ya saini zilikuwa ni za watu ambao hawana ardhi katika eneo lile.** Pia wanakijiji walieleza kuwa walilipinga wazo la huo mradi kwa mara ya kwanza lilipowasilishwa kwao, na kwamba walipojaribu kuizuia hiyo kampuni kwa njia za amani ili wasikate miti, kusafisha ardhi na kumiliki ardhi yao walitishwa na kuogopeshwa sana.

Wanakijiji pia walitueleza jinsi kampuni hiyo ilivyokuwa imetoa ahadi nyingi sana kwao, kwa mfano kampuni iliahidi kutoa ajira nzuri na kujenga shule kwa ajili ya watoto, lakini cha ajabu hakuna hata ahadi moja kati ya hizo iliyotekelezwa. **Ni watu wachache tu kati yao ndio walioajiriwa na kampuni tangu ilipoanza kufanya shughuli zake, na hadi wakati huo ulikuwa umeshapita mwaka mmoja bila wafanyakazi wake kulipwa mishahara yao.** Tulipovitembelea vijiji vingine vya jirani vilivyokuwa vimeathiriwa na mkataba huo wa ardhi, walitupa maelezo yanayofanana kuhusu jinsi kampuni ilivyoshindwa kutekeleza ahadi zake na jinsi ilivyoongeza umaskini na hali ya usalama mbaya wa chakula katika eneo lao.

Hata hivyo, wanawake wa kijiji cha Mamanka walivutiwa sana na habari waliyoisikia kuhusu mikutano ya viongozi wa jamii toka maeneo mbalimbali ya Sierra Leone pamoja na nchi

nyingine za Africa zilizoathiriwa na makampuni yanayoendesha mashamba ya michikichi ya mawese iliyofanyika wilayani Port Loko. **Walitambua kuwa hawako peke yao katika mateso wanayoyapitia na kwamba hatua zinaweza kuchukuliwa kuidai ardhi yao.**

Mwishoni mwa mikutano mingi, wanawake na washiriki wengine toka kijiji cha Mamanka waliazimia kuwa na madai rasmi kwa kampuni: kuwa ardhi yao irudishwe; na kwamba mishahara na kodi ya pango la ardhi ambayo haijalipwa ilipwe; na kwamba mikataba ya ukodishaji wa ardhi ibatilishwe na kufutwa. Mashirika yote 36 yaliyoshiriki katika mkutano yalisaini tamko la pamoja kuunga mkono madai hayo ya wananchi.

Kwa mujibu wa chifu mwanamke wa Kijiji cha Mamanka, Yarbom Kapri Dumbuya (zamani akijulikana kama Mamasu Dumbuya) alieleza kuwa mapambano ya kudai ardhi yao yalizidi na kuimarika baada ya mikutano hii. Alimweleza Aminata Finda Massaquoi wa Redio Culture wakati alipokitembelea kijiji hicho mwezi Novemba 2018 kuwa, **"Tulijifunza kutokana na uzoefu tuliousikia toka kwa wanawake wengine katika nchi yetu na ndani ya bara la Africa."**

Mapambano yao hatimaye yaliweza kupata uungwaji mkono toka shirika linaloshughulikia haki za kisheria linaloitwa NAMATI. Maofisa wa shirika hilo waliitembea jamii hiyo na wakakubali kuwasaidia kwa msaada wa kisheria ikiwemo uwakilishi wa kisheria ili kuipeleka kampuni hiyo mahakamani. **Baada ya kuhudhuria vipindi kadhaa mahakamani, mahakama iliamua na kuipatia haki jamii, na kisha ikatoa amri ya kimahakama kwa kampuni ya Sierra Leone Agriculture Ltd kurudisha ardhi yote kwa vijiji vya wilaya ya Port Loko na kisha kuwalipa fedha dola za kimarekani 250,000 kama kodi ya pango la ardhi iliyokuwa haijalipwa.** (7)

Huku wakitokwa na machozi, wanawake wa Mamanka walimweleza Aminata jinsi walivyopata ahueni baada ya kuipata ardhi yao na jinsi walivyofurahia kutembea juu ya ardhi yao pasipo manyanyaso. Waliwashukuru wote waliosimama pamoja nao wakati wa mapambano yao.

Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi ambazo zipo kwa upande wa wanajamii. Kampuni iliwaacha wakiwa na kisima hatarishi ambacho kilikuwa kimekamilika nusu yake tu huku takribani hekta 1,500 ya ardhi yao ikiwa imegubikwa na michikichi ya mawese. Wanakijiji wa Mamanka hawaelewi cha kufanya kwa uhakika kuhusiana na mashamba hayo ya michikichi ya mawese. Wanajiuliza, je waiondoe hiyo michikichi na kisha kupanda mazao ya chakula? Je, waunde ushirika ili waendelee kuzalisha mafuta ya mawese wao wenyewe? Je, kuna namna wanavyoweza kuyaunganisha mambo yote hayo mawili kwa pamoja?

Kampuni moja inayoweza kuwasiliana na wanavijiji wa Port Loko na kujaribu kuwashawishi na kuwalaghai ili wasaini mikataba mipya ni kampuni ya kidachi inayoitwa Natural Habitats *(Kwa Kiswahili: Makazi Asilia)*. Ni kampuni yenye mashamba ya michikichi ya mawese katika nchi hiyo, pia kampuni hiyo imeanzisha utaratibu wa kilimo cha mkataba na wakulima ili waweze kuzalisha mawese asilia yaliyoidhinishwa na kuthibitishwa. Kutokana na utaratibu wa kampuni hii, mara nyingi kampuni hii imetajwa kuwa ni kampuni bora kuliko makampuni makubwa yenye mashamba makubwa. Lakini wanakijiji wa Port Loko wanapaswa kuwa waangalifu na wawe na tahadhari. Ndugu Kevin Godlington, ambaye ndiye mtu aliyesababisha uwepo wa mikataba mibaya ya ardhi miaka kumi iliyopita, ndiye Afisa Mkuu wa Kampuni ya Natural Habitats! (8)

Ushindi wenye ujasiri wa wanakijiji wa Port Loko uliowawezesha kuipata ardhi yao ni kichocheo kwa jamii nyingine zilizoathiriwa na mashamba ya michikichi ya mawese katika nchi mbalimbali barani Afrika na duniani kote, ikiwemo wale wanaokabiliana na uporaji wa ardhi uliofanywa na kampuni ya Siva Group. Kwa sasa mapambano mapya

yanaanza kwa wananchi wa Port Loko ili kuhakikisha kuwa hawapotezi umiliki wa ardhi yao kwa mara nyingine tena.

Kwa sehemu makala hii imetumia taarifa toka kwa Aminata Finda Massaquoi kufuatia safari yake aliyoifanya katika kijiji cha Mamanka mwezi Oktoba 2018.

(1) Unaweza kuiangalia baadhi ya mikataba hiyo kwa kufuata kiungo hiki: https://www.farmlandgrab.org/post/view/22876-land-deals-in-sierra-leone-involving-kevin-godlington
(2) GRAIN, "Feeding the one percent," 7 October 2014: https://www.grain.org/e/5048
(3) Caitlin Ryan, "Large-scale land deals in Sierra Leone at the intersection of gender and lineage", Third World Quarterly, Vol. 39, 2018: https://www.tandfonline.com/doi/full/10.1080/01436597.2017.1350099
(4) Mahojiano yaliyofanywa na Joan Baxter na kisha yakawasilishwa kwa GRAIN, 2013
(5) Azimio la Porto Loko: Wanawake wanasema "Tunazitaka Ardhi Zetu Zirudishwe!", https://www.grain.org/e/5788
(6) Unaweza kuuona mkataba wa ardhi kwa kufuata kiungo hiki: http://farmlandgrab.org/uploads/attachment/Sla_Bkm_1.pdf
(7) Cooper Inveen, "Sierra Leone ruling against palm oil company will empower communities – campaigners," Reuters, 12 November 2018: https://farmlandgrab.org/28563
(8) https://www.natural-habitats.com/about/team/

Kuuhuisha Ustawi: Vijiji vya Kochi taluka, nchini India, wanapinga uchimbaji wa madini na wanafungua nafasi kwa ajili ya uongozi binafsi (1)

Ph.: Neema Pathak Broome

Mikutano ya vijiji *(Kwa Kihindi: Gram Sabhas)* huko Korchi *taluka*, wilaya ya Gadchiroli, jimbo la Maharashtra, India, pamoja na upinzani wa wanajamii dhidi ya uchimbaji madini unaofadhiliwa na serikali ya jimbo, wanafanya kazi ya kuzihuisha na kuzijenga upya taasisi za kiuongozi za serikali za mitaa. Mikutano ya vijiji *(Gram Sabhas)* 90 kati ya 133 katika eneo la Korchi *taluka* (*Taluka: ni aina fulani ya ngazi ya usimamizi wa serikali)* zimeungana na kuunda shirikisho la mikutano ya vijiji wanaloliita kwa lugha ya kihindi *Maha Gramsabha* (Maana yake *Gram Sabha kubwa*).

Wakati huo huo, muungano wa vikundi vya wanawake pia vimeanza kuzipasa sauti zao ili ziweze kusikika sio tu kwa lengo la kupinga uchimbaji madini bali pia kupinga aina mpya za ufanyaji maamuzi katika taasisi za ngazi za vijiji na *taluka,* ikiwemo *Maha Gramsabha*. Vikundi hivi vinajitokeza kama majukwaa ya kupinga uchimbaji madini, kupanga mikakati, kupanga masharti na kanuni za usimamizi wa misitu na uhifadhi, kumiliki njia mbalimbali zinazowawezesha kuishi pamoja na vyanzo vingine vya kiuchumi, kufufua utambuzi wao wa

kiutamaduni, kukuza usawa wa kijamii, kupaza sauti moja kwa moja na kukuza demokrasia ya kijinsia, na kuhoji mifumo iliyopo ya maendeleo. Makala hii inajaribu kuonyesha jinsi mchakato huu unavyozidi kujifunua.

Upinzani na Kujipanga toka ngazi za chini

Pamoja na kuwa watu wanasimamiwa na utawala wa Wilaya ya Gadchiroli ikisaidiana na *Panchayats* waliochaguliwa (Panchayats maana yake ni kamati tendaji inayohusisha kijiji kimoja au zaidi ambayo ndiyo kitengo cha kwanza cha utawala katika mfumo wa kiutawala wa India uojulikana kama Panchayati Raj, yaani serikali za mitaa zinazojitegemea), watu wa Korchi *taluka* wameendelea kuwa na aina zao nyingine za kiusimamizi ambazo si rasmi na ambazo ni za kimila zinazoitwa *Gram Sabhas* na *Ilakas* (zinazohusisha maeneo yanayohusisha vijiji vingi), mifumo hii isiyo rasmi ya watu wa Korchi inasimama kama miundo ya kiuongozi katika ngazi ya kijiji na ngazi ya juu ya kijiji. Hali zikiwa na mamlaka kidogo ya kisiasa na kiuchumi, taasisi hizi ambazo si rasmi hadi hivi karibuni zilikuwa zimejikita katika masuala ya kijamii na kiutamaduni na katika kusuluhisha migogoro. Eneo la Korchi *taluka* lina taasisi hizo zisizo rasmi yaani *Ilakas* tatu ambazo ni Kumkot, Padyaljob, na Kodgul; zikiwa na jumla ya *Gram Sabhas* 133 zenye wakazi wapatao 43,000 (kati ya hao asilimia 73 ni kutoka jamii za makabila ya kiasili ya Gond na Kanwar).

Karibia asimilia 85 ya wilaya ya Gadchiroli imegubikwa na misitu. Na takribani watu wote wanaoishi katika eneo hilo wanategemea sana misitu kwa maisha yao kwa maana ya kupata fedha na pia kupata chakula cha kujikimu. Pamoja na kuwa misitu ni ya maana sana kwa ajili ya uchumi wa watu wa chini na kwa maisha yao, bado misitu hiyo hiyo ni sehemu muhimu sana ya maisha ya kijamii na kidesturi kwa watu wa kabila la kiasili la *adivasi,* pia ni sehemu ya utambulisho wao wa kisiasa. Pamoja na ukweli huo hadi hivi sasa watu wengi katika eneo hilo wamewekewa vikwazo na wanaruhusiwa kutumia hiyo misitu kwa mbinyo kwa sababu ya utaratibu wa kikoloni unaotokana na sera na sheria zake za usimamizi wa misitu, kumekuwepo na ukiritimba ambao umesababisha desturi ya rushwa na maovu kwa mtu anayetaka kuutumia msitu. Misitu hii pia ni muhimu sana kwa serikali ya jimbo. Uziduaji wa kukata mbao kibiashara na mazao mengine ya msituni vimekuwa vikifanyika na idara ya misitu kupitia ukodishaji kwa wakandarasi na kwa makampuni ya karatasi na rojorojo za miti za kutengenezea vifaa vya ujenzi, na hivi karibuni ukodishaji umekuwa ukifanyika kwa makampuni ya uchimbaji madini.

Kwa miongo mingi, watu wa Gadchiroli wamekuwa wakizipinga sera kandamizi na zenye ubaguzi, pamoja na rushwa na maovu yanayofanywa kwa makabila ya wenyeji. Na pia wanapinga uchimbaji wa sasa wa madini unaofadhiliwa na serikali ya jimbo. Kati ya mwaka 1990 na 2017, leseni 24 za ukodishaji kwa ajili uchimbaji wa madini zimetolewa au kupendekezwa na Wilaya, kwa pamoja leseni hizo zimeleta athari katika eneo la takribani hekta 15,000 za misitu mizito na zaidi ya hekta 16,000 zilizoathirika kidogo. Katika eneo la Korchi *taluka* pekee, takribani leseni 12 za uchimbaji wa madini zilipendekezwa pamoja na kuwepo upinzani mkubwa na imara toka kwa wananchi, matokeo yake ni kuwa leseni hizo ziliathiri zaidi ya hekta 1032.66.

Baada ya mapambano ya wananchi kwa muda mrefu katika sehemu mbalimbali za India dhidi ya sera za kibaguzi, kandamizi, na sera za upande mmoja toka juu hadi chini ikiwemo sera mbaya za uhifadhi; basi kufuatia mapambano hayo mwaka 2006 serikali ilisalimu amri na kulilazimu Bunge la India kupitisha sheria ya kihistoria inayojulikana kama: Sheria ya Makabila Yaliyopangwa na Wakazi Wengine wa Kiasili wa Misituni, 2006 *(Kwa Kiingereza: The Scheduled Tribes and Other Traditional Forest Dwellers (Recognition of Rights) Act 2006*, pia sheria hii inajulikana kama Sheria ya Haki za Msitu ya India (*Kwa Kiingereza: Forest Rights Act of India (katika makala hii sheria hii itaandikwa kwa kifupisho hiki FRA)*. Sheria ya FRA imetoa mwanya wa kuzitambua aina 14 za haki mbalimbali za misitu za kiasili kwa makabila yaliyopangwa na kwa wakazi wengine wa kiasili wa misituni. Moja kati ya

mambo muhimu yaliyotambuliwa na sheria hii ni pamoja na ***Gram Sabhas* kuwa na haki ya kutumia, kusimamia, na kuhifadhi misitu yao ya kiasili na kuilinda misitu hiyo dhidi ya vitisho vya ndani na vya kutoka nje.** Sheria hii pia inalazimisha uwepo wa mashauriano huru, ya mapema kabla, na ridhaa yenye taarifa sahihi toka kwa *Gram Sabhas* kabla ya misitu yao ya kiasili haijabadilishwa matumizi kwa madhumuni ambayo si ya misitu. **Kati ya vifungu muhimu kabisa katika sheria hii na ambacho ni muhimu sana ni ufahamu mkubwa wa kutumia kitengo cha uongozi cha *Gram Sabha* –** ambacho kinaweza kutambuliwa na kikundi cha watu wanaoishi katika eneo ambalo linaweza lisiwe na sifa ya kuitwa kijiji katika rekodi za serikali.

Kuziwezesha Gram Sabhas

Baada ya kampeni endelevu inayohusu haki ya kutumia, kusimamia, na kuhifadhi misitu yao ya kiasili, kuanzia mwaka 2009 hadi 2011 *Gram Sabhas* 85 za Korchi *taluka* zilitambuliwa. Utambuzi huu ulisaidia kuziwezesha *Gram Sabhas* kusimamia misitu yao na kuitumia kwa namna ya uendelevu, kwa kuwa katika mazingira hayo ni dhahiri kuwa wananchi wanao umiliki wa misitu.

Baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa, hasa kutoka vijijini ambao wamepokea haki hizi maalum lakini ambao pia walikuwa wakikabiliana na vitisho toka kwenye miradi ya uchimbaji wa madini, walitumia fursa hii kufahamu jinsi sheria hii ya FRA inavyoweza kuziwezesha *Gram Sabhas*. Na pia **kuwahamasisha wananchi ili wafahamu jinsi *Gram Sabhas* iliyowezeshwa kisheria inavyoweza kufanya kazi kuelekea utambuzi binafsi na usimamizi binafsi, ikiwemo kudai mamlaka kubwa inayojali usawa katika kusimamia misitu na uchumi wa watu wa ngazi ya chini**. Mikutano ya kwenye ngazi ya *Taluka* inasaidia uwepo wa majadiliano ya kina kuhusu utendaji, haki, mamlaka, na majukumu ya *Gram Sabha*. Hadi kufikia mwaka 2017, vijiji 90 huko Korchi *taluka* walikuwa wamejipanga upya na kuziimarisha *Gram Sabhas* za vijiji vyao ili ziweze kuwa ni vyombo vyenye kufanya maamuzi shirikishi, na vyenye kuzingatia uwazi na uwajibikaji katika ngazi ya vijiji. Kila *Gram Sabha* ilifungua akaunti ya benki, walichagua katibu na mwenyekiti. Hawa wasimamizi wa ofisi wana majukumu ya kuwasiliana na maofisa wa serikali na wadau wengine wa nje. *Gram Sabhas* zilianza kujadiliana na kutangaza bidhaa zao za mazao ya msituni ambazo si mbao. Faida inayopatikana ilianza kwenda moja kwa moja kwa *Gram Sabhas*, ambayo iliwajibika kuwalipa wafanyakazi (familia zote katika kijiji), na walikuwa wanabakiza kiasi fulani cha asilimia kwa ajili ya akaunti ya kijiji na fedha iliyobakia iligawanywa kama faida kwa wakusanyaji wa fedha. Hadi wakati huo, *Gram Sabhas,* ambazo kimsingi zilikuwa zimedhoofika kiuchumi na kiuwezo zilianza kuyapata mambo hayo mawili, yaani uwezo na uchumi. Kwa mfano, mwaka 2014 *Gram Sabhas* zilikuwa na mapato sifuri, lakini ilipofika mwaka 2017, *Gram Sabhas* 87 zilikuwa na jumla ya mapato yaliyofikia zaidi ya Rupia milioni 120 (sawa na Dola za Kimarekani - US$ 1,700,000).

Hadi kufikia mwaka 2016, *Ilakas* za kimila zilianza kujiona kuwa zenyewe ni kama ngazi ya juu kuliko *Gram Sabha*s. Hivyo, hizi ***Ilaka* za kimila (Mikutano) zilianza kujumuisha majadiliano ya kuziwezesha *Gram Sabhas,* demokrasia ya moja kwa moja, kujitambua, sheria ya FRA, uchimbaji wa madini na athari zake, ukuaji na maendeleo, ukoloni na ubeberu, na mambo mengine.** Pia kulifanyika juhudi za kurejelea maana ya neno *'adivasi'* (kabila la kiasili), utamaduni wa *adivasi* na historia yake, na kuelezea kwa upya mapinduzi na mabadiliko ya mashujaa wa kikabila (historia ambayo haionekani katika historia za kawaida) na kufahamu ombwe la ufahamu kuhusiana na utamaduni na imani ya kabila la *adivasi* katika dini nyingine kuu.

Maha Gramsabha – Shirikikisho la Gram Sabhas

Kadri *Gram Sabhas* zilipoanza kupata nguvu kutokana na uwezeshaji na utambuzi, basi ilikuwa ni muhimu sana kwao kujiunga na kuwa na nguvu zaidi ili kuwasaidia wale ambao

walikuwa bado wanaanza ili wajipange na ili wawe na ufahamu wa pamoja na usaidizi. Ili kuvuna mazao ya misitu ambayo si ya mbao na kuweza kuyauza kunahitaji stadi na uelewa, ufahamu, na nguvu ili kuweza kukabiliana na nguvu ya soko. Lakini pia **ili kuweza kushughulikia mikakati inayoleta utengano ya makampuni ya uchimbaji wa madini kunahitaji kuwa na matendo ya nguvu ya pamoja.**

Ilaka sabhas za kimila zilikuwa na ukomo wake hasa katika kuyashughulikia mambo haya. Hivyo mwaka 2017, shirikisho la *Gram Sabhas 90* liliundwa ili kuhakikisha kuwa masoko hayawanyonyi wadhaifu, na ili kuwepo na usawa katika kugawana faida na kugawana maarifa, na ili kushikana mikono pamoja. Kwa sasa *Maha Gramsabha* (MGS) ni mahali pa kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni ambapo panalenga kutambuliwa na wananchi katika suala zima la utawala. Kila *Gram Sabha* inachagua wanawake 2 na wanaume 2 ili kuwa wakilisha katika MGS, pia kila *Gram Sabha* inapitisha azimio la kujiunga na MGS na kutii miongozo na kanuni zake. Wawakilishi wote waliochaguliwa wanatakiwa kutoa mrejesho kwenye *Gram Sabhas* wanazotoka. Na ikiwa kuna sera mpya imetolewa na MGS basi huwa inajadiliwa kisha hufanyiwa maamuzi kulingana na uelewa na taarifa walizonazo, lakini mambo hayo yote ni lazima yafikishwe kwenye *Gram Sabhas* kwa uthibitisho. Kabla ya kuikubali sera yoyote ile, wawakilishi hujadiliana juu ya mambo yanayohitaji utekelezaji na pia huwa kunakuwa na mjadala kuhusiana na gharama zilizotumika.

Wanawake, uchimbaji wa madini, na majukumu ya muungano wa vikundi vya wanawake

Katika jamii ya leo ambayo imeelemewa na mfumo dume, ni dhahiri kuwa wanawake hawana sauti kubwa katika vijiji vya kimila na katika usimamizi wa misitu. Pia wanawake walikabiliana na changamoto nyingi za kijamii, ikiwemo unyanyasaji na vurugu katika ngazi ya kaya ikichangiwa na ulevi, ukosefu wa rasilimali, na ukosefu wa haki katika kufanya maamuzi.

Hali wakiungwa mkono na AZAKI inayoitwa Amhi Amchi Arogyasaathi, taratibu kabisa vikundi vya wanawake *(parishads)* vilianza kufuatilia utekelezaji wa sheria na mipango ambayo itasaidia kuwawezesha wanawake. Vikundi hivi vya wanawake - *parishads* vilijikuta vinakuwa ni kundi kubwa la kuwasaidia wanawake wanaokabiliana na ukiukwaji wa haki, unyanyasaji, vurugu na mambo mengine yoyote yale katika ngazi ya familia au jamii kwa ujumla. **Kadri uelewa ulivyozidi kuongezeka miongoni mwa wanawake, na kadri walivyozidi kupata ujasiri wa kupaza sauti na kutoa maoni yao, hapo ndipo wanawake wengi sana walipoweza kusema hadharani kuwa ustawi wao na wa familia zao unahusishwa sana kwa karibu na ustawi wa misitu. Hivyo, ilikuwa ni lazima kwa wanawake kujadili suala la uharibifu wa misitu na haki ya kuweza kuitumia misitu na kuilinda.**

Jambo hili lilionekana kuwa ni muhimu sana kwa wanawake mwaka 2009, hasa katika vijiji ambavyo viligundua kuwa misitu yao ya kiasili imetolewa na kukodishwa kwa ajili ya uchimbaji wa madini. Kupitia vikundi hivyo - *parishads,* wanawake walikuwa ni sehemu ya nguvu kubwa ya upinzani dhidi ya uchimbaji wa madini. **Upinzani wao wa kimwili na uwezo wa kujieleza katika mikutano mbalimbali dhidi ya uchimbaji wa madini, ikiwemo mashauri yaliyokuwa yamefadhiliwa na serikali, basi jitihada hizo zote zilisababisha vibali vya ukodishaji kwa kazi ya uchimbaji wa madini kusimamishwa hadi leo hii huko Korchi *taluka***. Hatimaye, kupitia vikundi vyao *parishad,* wanawake waliweza kuwa na majadiliano kadhaa kuhusiana na athari za uchimbaji wa madini katika maisha yao, familia zao na misitu yao, ikiwemo haja ya kuilinda misitu. Pia vikundi hivyo vya *parishads* vimekuwa ni muhimu sana katika kuwakuza na kuwainua wanawake viongozi katika majukwaa mbalimbali ili kuelezea mapambano yao na maoni yao, ikiwemo fikra yao kuhusu ustawi, ambayo inahusishwa kwa ukaribu kabisa na misitu yenye afya.

Wakati wa kipindi cha upinzani dhidi ya uchimbaji madini katika eneo la Korchi *taluka,* wanawake viongozi katika vikundi vya *parishads* walianza kutambua na kujadili kuhusu uhalisia uliokuwepo ambapo wanawake wanakuwa mstari wa mbele katika upinzani ilhali hawana nafasi katika utaratibu wa kimila unaohusisha mchakato wa maamuzi kuhusu misitu. Hadi kufikia mwaka 2015, majadiliano kwenye ngazi ya *Gram Sabhas* kama vitengo vya uongozi vilikuwa vinaanza kupata nguvu, katika kipindi hicho mikutano ya ngazi ya *taluka* ilikuwa inaandaliwa, utekelezaji wa sheria ya FRA ulikuwa unazungumziwa katika ngazi mbalimbali za mikutano ya *taluka* na *Ilaka*. Hata hivyo, hakuna aliyekuwa anaangalia masuala ya ushiriki wa wanawake, haki za wanawake chini ya sheria hiyo na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kutokana na mazao ya misitu. Baadhi ya wanawake viongozi walianza kushiriki katika mikutano ya ngazi ya *taluka*.

Katika moja ya mikutano ya kwanza ya *Maha Gramsabha*, wanachama wa *parishad* walisisitiza kuwa **pamoja na kupinga ukiritimba unaoletwa na matabaka kandamizi, ilikuwa ni muhimu pia kupinga mifumo ya mila na desturi iliyokuwa ina halalisha maonezi kwa wanawake ikiwemo kuwazuia wanawake katika ufanyaji wa maamuzi, ikiwemo maamuzi kuhusiana na misitu.** Walihakikisha kuwa MSG inajumuisha wawakilishi 2 wanawake na wanaume 2 toka katika kila *Gram Sabha*. Kitendo cha kuwa na kitengo cha kwanza cha maamuzi cha *Gram Sabhas* katika vijiji vyao kulitoa fursa zaidi ya ushiriki wa wanawake kuliko muungano wa vikundi vya wanawake pekee yaani *parishads*, ambao uko mbali na kijiji. Kupitia juhudi zilizofanywa na *parishads,* baadhi ya *Gram Sabhas* zimefanya juhudi ya kipekee kuhakikisha mikutano inafanyika wakati ambapo wanawake wanaweza kushiriki. Vikundi vya wanawake vya *parishads* pia vilihakikisha kuwa Korchi *taluka* ni moja kati ya ngazi chache za kiutawala nchini ambapo haki za wanawake kwa mujibu wa sheria ya FRA zinazingatiwa. Sheria ya FRA inatoa mwanya na uwezekano wa kumiliki ardhi kwa pamoja kati ya mke na mume. Katika vijiji vingi vya Korchi, hati nyingi za umiliki wa ardhi zimetolewa kwa pamoja ikiwemo baadhi ambazo zipo kwa majina ya wanawake kama wamiliki wa kwanza na mahali pengine wanawake kama wamiliki pekee wa ardhi.

Hali wakipiga hatua mbele, *Gram Sabhas* nyingi zimefanya maamuzi kuwa wanawake watapata mshahara wa kila siku kwa kazi wanazofanya pamoja na faida toka kwenye mauzo ya mazao ya msituni ambayo si ya mbao moja kwa moja katika akaunti zao badala ya fedha hizo kulipwa katika akaunti za waume zao. Kusema kweli, kijiji kimoja kinachoitwa Sahle kimeamua kuwa faida yote inayopatikana katika familia toka katika mazao ya misitu itaenda katika akaunti ya wanawake wa familia hiyo – maamuzi ambayo ni makubwa na ya kipekee.

Hitimisho

Mchakato wa kudai haki, utawala na uongozi binafsi na usimamizi wa misitu katika eneo la Korchi bado upo katika hatua zake za awali na unazidi kujifunua vizuri na kwa usawa. Mambo kadhaa ambayo yamekuwa ni chachu ya kusaidia mchakato huo yamesaidia sana katika kuimarisha upinzani, utawala binafsi, ikiwemo madai ya dhana ya ustawi wa jamii katika eneo la Korchi. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na **historia ndefu ya kujipanga kisiasa na mijadala kuhusu 'maendeleo', jambo ambalo limetoa nafasi kwa uongozi imara wa ngazi ya chini wa wanaume na wanawake; uwepo wa viongozi wa kipekee ambao wamesababisha uwepo wa mijadala ya kiitikadi na hotuba mbalimbali; uwepo wa nafasi za kisheria zilizotolewa na sheria wezeshi kama ile ya FRA; kubadilishana uzoefu kati ya watu na watu; faida kubwa za kiuchumi baada ya kuugatua uchumi wa mazao ya misitu ambayo si mbao kwenye ngazi za chini; usaidizi wezeshi na usio ingilia toka mashirika mbalimbali na wanaharakati binafsi**.

Mambo hayo yamesababisha uwepo wa umakini wakati wote, wepesi, na mchakato unaohusisha vitu mbalimbali katika kushughulikia changamoto za ndani na za nje. Hii inajumuisha kushughulikia sera kandamizi na za kitabaka, ikiwemo matumizi ya nguvu nzito za kijeshi na sera za uchumi mpana ambazo zinaegemea na kuyapendelea makampuni na

kupendelea ubinafsishaji; ikiwemo kushughulikia matabaka na mfumo dume katika ngazi za chini. **Kujumuisha sauti za wanawake katika ufanyaji maamuzi na katika mgawanyo wa faida kumesaidia kuwepo kwa uongozi wa kijamii wenye usawa, na hivyo kumefanya kuwepo na upinzani imara dhidi ya uchimbaji wa madini, na usimamizi imara wa misitu na uhifadhi wake, na pia kumejitokeza dhana iliyo nzuri kuhusu ustawi wa wanajamii kama mbadala wa mfumo wa maendeleo unaojikita katika tasnia ya uziduaji.**

Neema Pathak Broome, Shrishtee Bajpai na Mukesh Shende
Neema na Shrishtee ni wanachama wa Kalpavriksh, wanaishi Pune na Mukesh na wanafanya kazi na asasi ya Amhi Amchi Arogyasaathi, asasi iliyopo Gadchiroli

(1) Makala hii imejikita katika uchunguzi wa muda mrefu uliofanywa na Kalpavriksh, kwa ushirikiano na asasi ya Amhi Amchi Arogyasaathi (AAA) na Korchi Maha Gramsabha kama sehemu ya mradi wa Maarifa Yaliyotolewa na Wanaharakati-Wanazuoni kwa Ajili ya Haki ya Mazingira *(Kwa Kiingereza: ACKnowl-EJ (Academic-Activist Co-Produced Knowledge for Environmental Justice)*. ACKnowl-EJ ni mtandao wa wanazuoni na wanaharakati ambao wanashughulika katika kuchukua hatua za utafiti shirikishi unaolenga kuibua mbinu nzuri za kuibadilisha jamii kama mbadala wa tasnia ya uziduaji (http://acknowlej.org/)

Upinzani wa Wanawake Walinzi wa Maeneo kwa Tasnia ya Uziduaji huko Amerika ya Kusini

Ph.:Cristina Chiquin

Huko Amerika ya Kusini, wanawake wamekuwa ni sehemu ya historia ya mapambano katika harakati za kulinda maeneo yao na mazingira. Kwa kupitia maandamano yaliyoratibiwa na vitendo vingine vya kila siku, wanawake hao wameweza kuzuia namna mbalimbali za uziduaji na aina mbalimbali za vurugu dhidi ya wanawake. **Pia wamekuwa mstari wa mbele katika mapambano kama hayo, huku "wakitumia miili yao" kuzuia uharibifu wa maeneo yao, pia wametoa mawazo muhimu kuhusu mfumo-dume na hali ya ubaguzi iliyomo katika tasnia ya uziduaji.** Kwa kutumia mkazo na tamko la wanawake kuwa "nafsi binafsi ni ya kisiasa" **wameweza kuhoji vitendo vya ngono katika mavuguvugu ya kijamii, ukandamizaji wa kijinsia na majukumu ya kijinsia, na wameweza kutengeneza nafasi yao inayojitegemea kwa misingi ya mshikamano na hali ya kujaliana kwa pamoja.** Katika makala inayofuata tutawashirikisha kuhusu tafakari kadhaa kuhusiana na mapambano ya wanawake hao, na tutatoa kwa ufupi juu ya hali ilivyo hivi sasa kuhusu mfumo wa tasnia ya uziduaji katika eneo hilo na madhara yake ya kipekee kwa maisha ya wanawake.

Tasnia ya uziduaji ni mfumo wa kiuchumi na kisiasa ambao misingi yake ni katika uundaji bidhaa na unyonyaji wa rasilimali usio zuiwa. Huko Amerika ya Kusini tasnia hii imeenea

sana tangu miaka ya 1990. Tasnia hii ya uziduaji inaleta uharibifu ambao ni mgumu sana kuurekebisha kwa kuwa inachafua hewa, ardhi, na vyanzo vya maji na inasababisha upoteaji mkubwa wa bayo-anuai. Zaidi ya yote, tasnia hii inaingilia na kugongana na haki za pamoja za wanajamii, inaharibu mbinu mbalimbali za kiasilia za kimaisha na za kiuchumi za wanajamii, na hatimaye inawafanya wanajamii hao kuwa tegemezi wa masoko ya nje.

Tasnia ya uziduaji, katika namna zake mbalimbali, imegubikwa na uporaji na matumizi ya mabavu kinyume na sheria. Tasnia hii ina msingi wake katika ubaguzi ulio ndani ya mfumo na unaojidhihirisha kupitia unyang'anyaji wa maeneo ya watu ya kiasili, pia unaojidhihirisha kupitia tabia yao ya kukana maisha ya kidesturi ikiwemo namna ambazo makabila ya kiasili, wazawa wa kiafrika, na wanajamii wa visiwani waliochanganya asili zao (*Raizales*) wanavyofanya katika kulinda mazingira.

Jinsi gani tasnia ya uziduaji inavyofanya kazi Amerika ya Kusini?

Huko Amerika ya Kusini na maeneo ya Karibeani, tasnia hii ya uziduaji imejikita katika uporaji na vurugu ambapo madhara yake hasi na mabaya yanaonekana bayana, pia tasnia hiyo imegubikwa na mikakati mibaya inayofanywa na makampuni katika kunyang'anya ardhi na maeneo mengine kwa ushirikiano na serikali mbalimbali katika nchi ambazo shughuli hizo zinafanyika, na mara nyingi mambo hayo yanafanyika kwa ushirikiano na serikali za nchi ambako kampuni husika inatoka.

Ushirikiano wenye hila kati ya makampuni, serikali mbalimbali, na katika mazingira fulani uhusishwaji wa makundi haramu yenye silaha na mabavu mengine yanayofichwa, ni vitu vinavyoweza kuonekana sana katika hatua mbalimbali zinazohusisha migogoro mbalimbali ya kijamii na kimazingira kama ifuatavyo: a) sheria na sera zinazo wapendelea wawekezaji na makampuni katika nchi zinazolengwa; b) ukiukwaji wa haki ya kuwa na majadiliano ya kabla, yasiyo na masharti, na yenye taarifa za mapema na ushiriki wa asasi za kiraia, hali ambayo inaruhusu miradi kuanzishwa hata kama kuna upinzani wa wanajamii; c) ulinzi wanaopewa makampuni na vifaa vyao kwa kupitia uwekaji wa vifaa vya **kijeshi** katika maeneo huku ulinzi huo ukisimamiwa na makundi yenye silaha na uhalifu unaoratibiwa; na d) uingiliaji wa majaji, mahakimu, na waendesha mashtaka wanaokana kuwa makampuni hayo hayahusiki, na hivyo kusababisha hali ya kutojali kuadhibiwa kuendelea kuwepo.

Kwa sasa, Amerika ya Kusini inaendelea kuwa moja ya eneo lenye hatari sana kwa wale wanaojaribu kulinda maeneo yao: **Asilimia 60% ya mauaji ya watu wanaolinda ardhi na mazingira katika maeneo yao duniani yamerekodiwa kufanyika katika eneo hili.** Kwa mujibu wa ripoti ya hivi karibuni iliyochapishwa na asasi ya kimataifa ya ushuhuda inayojulikama kama *(International NGO Global Witness)* nchi ambazo zina kiwango cha juu cha mauaji hayo kipo katika nchi za Brazili, Kolombia, Honduras, Guatemala, Peru na Nicaragua. (2)

Moja ya mkakati unaotumiwa na makampuni na serikali katika kuzimisha upinzani ni kuwabambikizia watu mashtaka ya jinai, jambo hili linafanyika sana katika miradi yote mikubwa ya uziduaji. Jambo hili linatokea kwa kuwanyanyapaa wapinzani, kuwaharibia sifa katika vyombo vya habari au kupitia matamko ya maofisa wa serikali, ukandamizaji wa maandamano ya kijamii na matumizi ya madai ya kisheria au mashtaka ya jinai kwa watetezi wa wanajamii na mazingira. Hali hii inathibitisha uwepo wa mfumo wa sheria wenye upendeleo na usio zingatia haki na usawa kwa wote: wakati makampuni yanapofurahia usalama wa kisheria na ulinzi wa silaha katika harakati zao za kuyachukua maeneo yote, wale wanaopambana kuyalinda na kuyatetea maeneo yao wanateswa na kupewa vifungo vibaya kwa uonevu.

Ni jinsi gani wanawake wanaathirika kipekee?
Tasnia ya uziduaji imejikita katika kuendeleza mfumo dume, mfumo ambao una athari za kipekee kwa njia mbalimbali za kimaisha kwa wanawake. Kama ambavyo baadhi ya wataalamu wa kike na watetezi wa ardhi wanavyodai, kuna uhusiano wa kidesturi, kihistoria, na mifano mbalimbali inayoenda sambamba kati ya unyonyaji na hali ya kuitawala miili ya wanawake na mazingira ya kiasili. Kwa mfano, katika muktadha wa uchimbaji madini na uchimbaji wa mafuta na uwekezaji wa mabwawa ya maji ya kuzalishia umeme, hali ya 'kudumisha mfumo-dume' katika kumiliki na kutawala maeneo na ardhi kunafanyika kwa makusudi (3) ambapo nafasi ya jamii na maisha ya kila siku yanabadilishwa ili kukidhi matakwa na mahitaji ya kundi moja la kijinsia la wanaume lenye mfumo-dume.

Watetezi wa haki za ardhi na wanawake wanathibitisha kuwa vitendo vya kutoweka kwa ardhi na uchafuzi wa maeneo vinatokea huku vikiandamana na kurudi kwa vurugu za wanaume dhidi ya wanawake na wasichana ikiwemo kuongezeka kwa ukosefu wa usawa wa kijinsia. Mambo hayo yanatokea katika maeneo yote ya maisha yao na yanaweza kuthibitishwa kutokana na uwepo wa mambo yafuatayo: a) ongezeko la mzigo wa kazi kwa maana ya majukumu yanayofanywa na wanawake; b) kupotea kwa uwezo na uhuru wa kiuchumi na usalama wa chakula; c) kuongezeka kwa vurugu za kisaikolojia, kimwili, kiuchumi, mfumo-dume na vurugu za kingono katika muktadha wa familia na jamii; d) ongezeko la athari mbaya za kimwili, kihisia na katika afya ya uzazi kutokana na uchafuzi wa hewa, ardhi na maji; e) ubaguzi kwa msingi wa kijinsia na ukiukwaji wa haki za ushiriki wa wananchi kwa msingi wa kanuni inayozingatia mchakato wa ushirikishwaji wa kabla, pasipo masharti, na wenye taarifa za mapema (4); f) kuongezeka kwa unyonyaji wa kingono kwa wanawake na wasichana na; g) kupotea kwa utambulisho wa kiutamaduni na kudhoofika kwa majukumu ya kiasili ya wanawake katika jamii.

Vurugu dhidi ya wanawake walinzi wa maeneo
Hatari maalum na ambayo imekuwa ikiwakumba wanawake walinzi wa maeneo mara kwa mara ni nyongeza tu ya madhira ambayo wanawake wamekuwa wakikabiliana nayo kihistoria, mateso hayo yanatokea kutokana na uwepo wa mfumo wa kijamii ambao umegubikwa na kutokuwepo kwa haki na udhalimu wa kijinsia, ubaguzi, na matabaka. **Kinyume na ilivyo kwa wanaume, walinzi wanawake wanakabiliana na vurugu za aina mbalimbali, hasahasa unyanyasaji wa kingono.** Pamoja na kupata mashambulio toka kwa makampuni na mawakala wa serikali, walinzi hao wa kike wa maeneo wanakabiliana na vurugu mbalimbali kila siku katika muktadha wa familia na jamii zao, na mara nyingine wanakabiliana na vurugu hata katika mashirika yao na mavuguvugu mengine ya kijamii.

Ingawa takwimu za wanawake waliouawa ni ndogo ukilinganisha na zile za ndugu zao wanaume, ni muhimu kuuangazia uhalisia uliopo katika uchunguzaji wa kesi za "mauaji ya wanawake wanaolinda maeneo yao" kama wanawake walinzi wa maeneo wa Guatemala wanavyouita uuaji huo *"Kwa Kiingereza: territorial femicides,"* (6) ni dhahiri kuwa uchunguzi wa mauaji ya wanawake unashughulikiwa tofauti na ule wa wanaume. **Kutokuwepo kwa utambuzi wa kazi ya wanawake watetezi na upendeleo wa mamlaka za kisheria wanaotumia chuki dhidi ya wanawake na upendeleo wa kibaguzi unasababisha kesi zao nyingi kuchukuliwa kuwa ni "uhalifu unaotokana na wivu wa kimapenzi," na hivyo kudharau muktadha wa upinzani unao ongozwa na wanawake kama hao na wakati mwingine hata kubuni na kutunga kuwa kesi za jinsi hiyo ni za kujiua na kujitoa mhanga**, jambo ambalo kimsingi linasabibisha na kuimarisha hali ya kutojali na kutoogopa kuchukuliwa hatua. (7)

Kwa sababu hiyo, vurugu za jinsi hiyo haziishi kwa kuuondoa uwepo wa kimwili wa wanawake watetezi: namna ambavyo uchunguzi unafanyika, au kwa lugha nyingine kuwafanya wanawake waonekane waovu, na kuwageuza ili wawe watu wabaya, na kuzuia haki na malipo kwa wanawake hao na familia zao hakusaidii chochote katika kumaliza vurugu dhidi ya wanawake.

Pia vurugu tofauti zimesababisha uwepo wa madhara tofauti katika maisha ya wanawake watetezi. Athari hizo mbaya ni pamoja na za kimwili, kihisia na kuathirika kwa afya ya kiroho, madhara ambayo huonekana kupitia hali ya kukosa usingizi, kupungua uzito, kujawa na hofu ya kudumu, msongo wa mawazo, na hata baadhi ya magonjwa hatarishi kama vile kansa. Pia matendo ya kubambikiziwa makosa ya jinai na kunyanyapaliwa yamekuwa na athari zilizo wazi katika shughuli zao za kiuchumi, na mara nyingi wamekuwa wakitengwa hata katika jamii na familia zao. Katika ngazi ya pamoja, vurugu hizi zinayadhoofisha mashirika yao, zinaleta hofu miongoni mwa wanawake na wakati mwingine zinasababisha mpasuko au mkwamo katika mapambano yao.

Mapendekezo toka kwa wanawake wa Amerika ya Kusini kwa ajili ya kuyalinda maeneo yao na kuondoa vurugu dhidi ya wanawake

Katika mfumo wa kazi yao kama watetezi na watunzaji wa mazingira na hali ya asili, wanawake wamejiundia matendo fulani ambayo yamesaidia katika kutoa msimamo na mitazamo yao juu ya madai kadhaa, na katika nyakati nyingi wanawake hao **wameweza kuzuia au kusimamisha shughuli kadhaa za uziduaji ambazo zinatishia maeneo yao.** Pia, **wameweza kuzalisha mabadiliko muhimu sana katika ngazi binafsi na pia katika ngazi ya pamoja,** wameweza kufanya hivyo kwa kutengeneza vitendo ambavyo vinalenga kuimarisha ulinzi na usalama madhubuti.

Moja kati ya hazina zao za vitendo vya kijamii ni pamoja na: a) kutengeneza nafasi kwa ajili ya mijadala na kubadilishana uzoefu wa namna ya kujilinda katika ngazi ya kitaifa na kikanda na katika kujenga mitandao ya kikanda ili kuimarisha hali ya kuonekana na kujulikana, kupata washirika, na kujenga vitovu vya upinzani katika ngazi ya chini ya jamii; b) kuandamana na vitendo vya upinzani vya moja kwa moja bila kupingwa ili kuzuia kusonga mbele kwa shughuli za uziduaji, na kuirejesha ardhi iliyoporwa: yaani matendo kama kufunga barabara, maandamano, kambi za kudumu ili kuzuia ufungaji mitambo ya kampuni; c) vitendo vya nguvu za kisheria ili kuamsha namna mbalimbali za ulinzi katika mfumo wa kitaifa na kimataifa, na pia shughuli za utetezi zinazolenga kuwafikia viongozi wa serikali za mitaa na mamlaka za kitaifa, na kuyafikia pia mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu; d) kuandika ripoti zinazohusu vitendo vya vurugu na ubambikiziaji kesi kwa walinzi wa kike, na pia uundaji mikakati ya mawasiliano ili kuyafanya mapambano yao yaweze kusikika; e) kuhamasisha majadiliano huru na binafsi ili wanajamii waweze kuelezea nia na mawazo yao kuhusu maamuzi na vitendo vinavyoathiri mazingira yao, na haja ya kuwa na majadiliano ya kabla ya mradi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa; f) vitendo vya kila siku vya upinzani kwa lengo la kulinda usalama wa chakula – kupitia uhifadhi wa mbegu za asili na matumizi yake ya kiasili, vitendo vya kilimohai vinavyohifadhi ikolojia – ikiwemo njia mashuhuri inayojulikana kama uchumi wa kike wa mshikamano na g) vitendo na tafakari kuhusu namna ya kujilinda binafsi na namna ya kujilinda kwa pamoja, ikiwemo jitihada za uponyaji binafsi na uponyaji wa pamoja.

Moja kati ya michango mikuu ya mapambano ya wanawake na watetezi wa nadharia ya haki na usawa wa wanawake kwa ajili ya ulinzi wa ardhi na maslahi ya pamoja ni ule wa kukazia uhusiano uliopo kati ya miili na maeneo ya kuishi. **Watetezi wa wanawake wa Guatemala wameshauri uwepo wa hoja inayohusu *mwili-ardhi na eneo* katika kuyaangazia mapambano ya kulinda ardhi dhidi ya tasnia ya uziduaji, hoja imejikita kuwa mambo hayo mawili ni lazima yaende pamoja bila kutenganishwa katika mapambano ya wanawake katika maeneo hayo ili waweze kuishi maisha ya huru mbali na vurugu na unyonyaji wa miili yao.**

Kutokana na uzoefu wao kama watetezi wa ardhi, wanawake wameweza kulazimisha uwepo wa nafasi ya mabadiliko kwa msingi wa utunzaji na uangalizi wa uhai katika namna zake zote, ikiwemo jitihada jumuishi zinazo ongezeka katika kuitunza dunia na kujitunza wao

wenyewe kwa ujumla, na mambo hayo ni muhimu sana katika uanaharakati wao. Maono haya mapana ya utunzaji na uangalizi yanaonekana kwa namna ambavyo baadhi ya mashirika ya wanawake na yale ya makabila ya kiasili yanavyo itazama dhana nzima ya ulinzi: **ulinzi wa watetezi wa haki za wanawake na watetezi wa mazingira ni muhimu sana na mambo hayo yamefungamana na ulinzi wa ardhi na maeneo.** Kwa fikra hii, mashirika yanapendekeza hatua za ulinzi na vitendo vinavyojumuisha masuala ya kiroho ya makabila ya kiasili, wazawa wa kiafrika na jamii zilizochanganyikana za visiwani (*Raizales*). Katika muktadha huu, **uponyaji unakuwa ni jambo muhimu sana:** kutokana na mjadala wenye ufahamu tofauti kati ya watu mbalimbali, mazingira na vizazi tofauti, na kutokana na hatua ya kuzirejelea kumbukumbu za wahenga, **walinzi wa wanawake sio tu kwamba wanaleta uponyaji kutokana na athari mbaya za uvamizi walioteseka nao kutokana na uanaharakati wao wa mazingira, bali pia wanaponya majeraha makubwa ya kimfumo ya vurugu dhidi ya wanawake.**

Laura María Carvajal Echeverry, ni Mratibu wa Program ya Wanawake na Maeneo iliyo chini ya Mfuko wa Hatua za Haraka (Kwa Kiingereza: Urgent Action Fund) kwa ajili ya Amerika ya Kusini na Karibeani (8)

(1) Makala hii inatokana na chapisho letu linaloitwa “Tasnia ya Uziduaji Amerika ya Kusini. Athari kwa Maisha ya Wanawake na Mikakati ya Kulinda Maeneo – Kwa kiingereza: Extractivism in Latin America. Impacts on women's lives and strategies for the defense of territory," linalopatikana katika tovuti yetu kwa anuani hii: https://www.urgentactionfund-latinamerica.org/site/assets/files/1346/b81245_6cc6d3d7edd447d0ab461860ae1ae64f.pdf
(2) GLOBAL WITNESS, 2018. At what cost? Irresponsible business and the murder of land and environmental defenders in 2017. Available at: https://www.globalwitness.org/en/campaigns/environmental-activists/at-what-cost/
(3) See: CABNAL, Lorena. Without being consulted: the commodification of our body-land territory, in: Women Defending the Territory. Experiences of participation in Latin America. Urgent Action Fund of Latin America and the Caribbean, 2015, https://issuu.com/fondodeaccionurgente-al/docs/territorio_engl; and GARCÍA TORRES, Miriam. Feminism reactivates the struggle against 'extractivism' in Latin America. Published in La Marea on 17 February 2014, by the Latin American Network of Women Defenders of Social and Environmental Rights;, https://www.rebelion.org/noticias/2014/2/181047.pdf (Andiko hili linapatikana kwa Kihispania tu)
(4) Kwa mitazamo mipana kuhusu ushiriki mkamilifu wa wanawake katika masuala ya mazingira na kuhusu uzoefu wa wanawake katika nchi mbalimbali kwa msingi wa dhana ya uhuru wa majadiliano ya kijamii, tunaomba uangalie machapisho yetu ya pamoja na wanawake walinzi kutoka Argentina, Guatemala, Bolivia na Ecuador: Women defending the territory: experiences of participation in Latin America | 2015, chapisho linapatikana hapa kwa lugha ya kiingereza: https://issuu.com/fondodeaccionurgente-al/docs/territorio_engl
(5) Kwa mtazamo wa kina kuhusu ubambikiziaji wa kesi za jinai na mashambulizi dhidi ya wanawake walinzi wa maeneo, tazama Ripoti yetu ya Kikanda Kuhusu Aina za Jinai na Vikwazo vya ushiriki mkamilifu wa wanawake wanaolinda haki za mazingira, maeneo na uoto wa asili katika bara la Amerika inayopatikana hapa: https://fondoaccionurgente.org.co/site/assets/files/1348/ingles.pdf
(6) Aina hii ya uelewa imekuwa ikihamasishwa na wanawake walinzi wa maeneo, wakiwemo Red de Sanadoras del Feminismo Comunitario de Guatemala (Network of Healers of Community Feminism of Guatemala).
(7) Kwa mapitio na mtazamo mpana wa hali ya kutojali na bila kuogopa kuadhibiwa, tazama Ripoti yetu ya Kikanda Kuhusu Kutojali Vurugu dhidi ya Wanawake Walinzi wa Maeneo, Bidhaa za Pamoja, na Uoto wa Asili katika Amerika ya Kusini, 2018, inayopatikana hapa: https://www.urgentactionfund-latinamerica.org/site/assets/files/1343/regional_report_-_impunity.pdf
(8) Mfuko wa Haraka wa Amerika Kusini na Karibeani inayoongea Kihispania ni mfuko wa kikanda wa kike unaochangia kuleta uendelevu na kuwaimarisha wanaharakati na mavuguvugu yao, kwa lengo la kimkakati kwa kuzingatia hatari na fursa. Tunaunga mkono upinzani, mapambano na madai ya wanawake walinzi wa haki na maeneo katika harakati za kubadili mfumo usio na haki na usawa, kwa kusisitizia juu ya ulinzi wa wanawake watetezi: https://fondoaccionurgente.org.co/en/

Tafakari kutoka Afrika: Ishinde hofu ya kujenga vuguvugu imara la mabadiliko

Sekretarieti ya shirika la WRM International ilifanya mahojiano na mwanaharakati wa masuala ya kijamii na kimazingira na mtetezi wa haki za binadamu Ndugu Nasako Besingi. Yeye ni Mkurugenzi wa shirika la Kikameruni linaloitwa Struggle to Economize the Future Environment (SEFE) – *(Kwa Kiswahili: Mapambano ya Kuyalinda Mazingira ya Baadaye),* shirika hili linazisaidia jamii za vijijini katika mapambano yao ya kupata haki zao za ardhi dhidi ya makampuni ya mashamba makubwa ya michikichi ya mawese. Ndugu Nasako aliwaandaa wanajamii kuandamana na kupinga uendelezaji wa mashamba ya michikichi ya mawese kunakofanywa na kampuni ya kimarekani ya Herakles Farm. Kutokana na harakati hii, alijikuta akiwa ni mhanga wa kampuni ya Herakles Farm na akawa pia mhanga wa serikali akikabiliana na manyanyaso ya kushambuliwa kimwili, kutishiwa, na kubambikiziwa kesi za uhalifu. Mwanaharakati huyu alikemea na amekemea vikali ukiukwaji wa haki za binadamu katika ukanda unaozungumza lugha ya kifaransa nchini Kameruni.

Mara nyingi, utasikia maelezo kuwa jamii za Afrika haziwezi kuzilinda wala kuzidai ardhi zao toka kwa makampuni ambayo yamepata hati za kukodishiwa ardhi toka kwenye serikali za kitaifa, kwa kisingizio kuwa Sheria za kitaifa zinadai kuwa, "ardhi yote ni mali ya Serikali". Wewe una mtazamo gani katika hoja hii?

Jambo la kwanza la kutafakari ni hili, ni kitu gani kinachounda Serikali? Serikali ni lazima iwe na mambo makuu manne yafuatayo: watu, eneo la utawala, dola, na utawala. Hivyo sentensi inayosema kuwa, "ardhi yote ni mali ya Serikali" haimaanishi kuwa ardhi yote inamilikiwa na serikali, bali ina maanisha kuwa ardhi yote inamilikiwa na watu wote wanaoishi katika himaya ya Serikali husika, wakiwemo watu waliopo ndani ya serikali. Sehemu kubwa ya watu katika Serikali nyingi ni wale wanaoishi katika maeneo ya wananchi vijijini, ambapo kila siku wanapambana kuzilinda ardhi zao na maeneo wanayoishi. Kwa upande mwingine, serikali inaweza kuelezewa vizuri kuwa ni wakala ambaye ndiye msimamizi na ambaye DHAMIRA ya Serikali imeundwa juu yake, inatekelezwa, na kusimamiwa kupitia sera za pamoja ambazo zinafafanua juu ya mwelekeo na maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Ukiyatafsiri majukumu hayo hayaleti maana kuwa haki zote zipo juu ya serikali kuhusu ardhi pamoja na rasilimali zilizomo ndani ya Serikali.

Ni makosa kwa serikali yoyote ile kudai kuwa inamiliki ardhi, huku ikizitupilia mbali haki za wananchi kumiliki ardhi. Kwa hakika, tatizo lililopo katika sheria nyingi za ardhi barani Afrika zinatokana na ukweli kuwa ziliandikwa kwa usaidizi wa watawala wa kikoloni, ambao pasipo hata ridhaa ya wananchi, waliyakabidhi maeneo na himaya zote kwa maraisi, huku wengi wao wakiwa ni wale ambao hawakuchaguliwa na wananchi, yaani waliteuliwa tu na wakoloni ili kulinda maslahi ya wakoloni ya muda mrefu. Zaidi ya yote, dhana inayoeleza kuwa "ardhi yote ni mali ya Serikali" haiipatii serikali haki ya kumiliki ardhi na kisha kuitumia kadri

itakavyo, bali inaipatia serikali haki ya kuisimamia na kusajili masuala yote yanayohusu ardhi huku ikizingatia na kuheshimu maslahi ya wanajamii.

Ni jukumu la serikali zote kuhakikisha kuwa wananchi wake wanakuwa na furaha, uhuru na amani na pia ni sharti serikali ilinde mali na amana za watu. Kwa nyongeza, serikali hizi zimesaini na kukubaliana na mikataba ya kimataifa kwa niaba ya Serikali za watu ili kulinda haki za wananchi. Kwa kuwa sheria za kimataifa ziko juu kuliko sheria za kitaifa, itakuwa ni sahihi kueleza kuwa kitendo cha kusaini na kukubaliana na miongozo ya kimataifa kunazishinda nia za serikali kugawa ardhi kwa kutafsiri vibaya kifungu kinachosema “ardhi yote ni mali ya Serikali”, pasipo ridhaa toka kwa watu, ambao maisha yao ya kila siku yanategemea sana ardhi zao.

Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu, ambalo linapatikana katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Afrika kuhusu Watu na Haki zao, na mikataba mingine ya kimataifa linaharamisha vitendo vya serikali kuchukua ardhi kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo pasipo kupata ridhaa toka kwa wananchi. Hivi karibuni, Mahakama ya Kimataifa inayoshughulikia Uhalifu wa Kivita ilikuwa inatafakari juu ya uporaji wa ardhi na ukiukwaji wa haki za wananchi kama moja ya uhalifu unaopaswa kuangaliwa na kushughulikiwa katika ngazi ya kimataifa na ikaahidi kuwachukulia hatua wale wote wanaokiuka haki hizo za wananchi (kwa maana ya serikali mbalimbali na makampuni).

Tangu nilipoanza kujishughulisha na masuala ya haki za wananchi kuhusu ardhi kupitia mashirika mbalimbali na vuguvugu la mabadiliko nchini Kameruni na nchi zingine, sijawahi kukutana na jamii hata moja inayokubaliana na wazo au dhana kuwa ardhi inamilikiwa na serikali. Jamii nyingi zilieleza dhahiri na waziwazi kuwa ardhi ni mali ya jamii na urithi toka kwa wahenga wao. Hakuna hata jamii moja niliyofanya nayo kazi inayokubaliana na uwepo wa makampuni ya kimataifa katika ardhi zao, wananchi wanadai kuwa makampuni hayo yalianzishwa kwa mbinu za mabavu.

Kwa uzoefu wako, ni mambo gani muhimu/ama ni mikakati gani mizuri katika kujenga vuguvugu la mabadiliko na kuimarisha mapambano ya wananchi kwa kuzingatia muktadha wa Kiafrika?

Vuguvugu la mabadiliko na mapambano ya wananchi barani Afrika bado yapo katika hatua za awali kutokana na historia ya Afrika iliyogubikwa na giza la utumwa, ukoloni, ukoloni mambo leo uliojitokeza mara baada ya uhuru, huku kukiwa hakuna fursa za kidemokrasia na haki za binadamu. Leo hii hali inaonekana kuwa tofauti sana, huku kukiwa na demokrasia kwa kiasi fulani na matumizi kidogo ya haki za binadamu kunako shinikizwa na nchi zilizoendelea kiviwanda.

Jambo muhimu zaidi katika kujenga vuguvugu imara la mabadiliko barani Afrika ni kuishinda hofu na ujinga ulioingizwa kwa makusudi na utawala wa wakoloni na utawala wa kikoloni-mamboleo uliofuata baada ya ukoloni. Jambo jingine muhimu la kuzingatia ni kuainisha mahitaji ya jamii huku kukiwa na jitihada za makusudi za kukuza uelewa na miongozo yenye kutoa elimu kuhusiana na mahitaji hayo ya wananchi. Jambo jingine muhimu ni kuimarisha uwezo wa wanaharakati na watetezi wa wananchi na asasi za kiraia ili waweze kufahamu haki zao na namna ya kuzilinda kwa kuzingatia shughuli zao mbalimbali za kila siku za kimaisha. Ukweli ni kuwa vuguvugu la mabadiliko imara na la kudumu ni lile linalojengwa kutoka ndani na si nje, hii ina maanisha kuwa vuguvugu imara la mabadiliko ni lazime litokee ikiwa limezingatia changamoto za wananchi.

Baadhi ya mikakati ya kuweza kusonga mbele ni pamoja na: kuanzisha jumuiko imara la kiafrika la asasi za kiraia na wananchi barani Afrika kwa lengo la kupashana habari na uzoefu; kupanga na kutekeleza shughuli mbalimbali katika maeneo ya wananchi kuhusu haki za ardhi; kusaidia shughuli za ushawishi na uchechemuzi katika kulinda na kutatua vurugu

na ukiukwaji; kusaidia uwepo wa aina mbalimbali za vitu vinavyotoa elimu kwa wananchi; na hatua nyingine ni kutengeneza miongozo na video mbalimbali za taarifa katika lugha rahisi zinazoeleza na kufafanua mikakati na mbinu mbalimbali inayotumiwa na makampuni katika kujipenyeza na kuzifikia jamii na kisha kuzipora ardhi za wahenga wao.

Je, changamoto kuu ni zipi?

Katika muktadha wa Afrika, kuna changamoto nyingi sana ambazo zinahitaji mbinu tofauti ili vuguvugu la mabadiliko liweze kufanikiwa. Changamoto ya msingi sana hapa ni ujinga na hali ya wananchi wengi kutokuwa na ufahamu kuhusu haki za ardhi na jinsi ya kuzilinda ardhi za wahenga wao, na hii inatokana na kutokuwa na uwezo wa kupambana na kuzuia nguvu inayokuja kwao ikiwa na nia ya siri ya kunyang'anya ardhi zao kunakofanywa na makampuni na serikali mbalimbali. Changamoto nyingine ni uongozi mbaya uliogubikwa na rushwa na umaskini kwa lengo la kuwafanya wananchi kuyanyenyekea mapenzi ya serikali. Pia kuna vikwazo vya kisiasa ambavyo vinawekwa na serikali ili kuminya haki za NGOs, asasi za kiraia (AZAKI), pamoja na mavuguvugu mengine ya mabadiliko ya kijamii, kupitia vitisho na kubambikiziwa kesi za uhalifu. Pia mitandao inayoendesha vuguvugu la mabadiliko ni lazima iwe tayari kukabiliana na mazingira magumu na ukosefu wa fursa za rasilimali fedha.

Kwa mtazamo wako, unafikiri mshikamano wa kimataifa ni muhimu katika kusaidia mapambano ya wananchi?

Mshikamano wa kimataifa ni jambo pekee bora lililobakia ili kuweza kuzuia uporaji wa kijinga wa ardhi ya wananchi. Jambo hili ni la muhimu sana ili kuweza kumaliza ushirikiano wenye kificho kati ya makampuni na serikali mbalimbali kwa kutumia ujinga wa wananchi, kuwanyonya wananchi na hatimaye kupora ardhi zao.

Hatua ya kwanza muhimu ni upatikanaji wa elimu na ufahamu kuhusu haki ambako kutasababisha uwepo wa vuguvugu imara la kudai mabadiliko na kupinga wizi na uporaji wa ardhi. Kutoa elimu kupitia upashanaji habari katika ngazi ya chini ya wananchi, ambako ndiko ukiukwaji mkubwa unafanyika, na kisha kutoa taarifa za ukiukwaji katika zile nchi zinazotoa fedha kwa makampuni na nchi nyingine waliko wateja wa bidhaa zao.

Vikundi vya ngazi ya chini vinaweza visiwe na uwezo wa kuvishinda vitisho peke yao, vurugu na ukiukwaji, ikiwemo mlolongo wa kuzitupilia mbali na kuzikanyaga kesi za kisheria zinazolenga kuwashtaki serikali na makampuni. Mara nyingi vikundi hivi havina uzoefu wa kutosha wa kutumia mbinu zisizohusisha vurugu ambazo zinajumuisha mambo kama kuwa na ufahamu sahihi na akili ya kukabiliana na wale wanaokiuka na waonezi.

Ni aina gani ya mshikamano wa kimataifa unaofikiri umefanya vizuri hadi sasa?

Hadi sasa, na katika muktadha wa Kiafrika, ninaweza kuifikiria kampeni moja nchini Kameruni dhidi ya kampuni ya Herakles Farms, ambayo ni kampuni ya kimarekani ambayo ilikuwa imeazimia kukata na kusafisha hekta 73,000 za misitu ya asili safi kabisa ili iweze kuanzisha mradi wake wa mashamba ya michikichi ya mawese katikati ya maeneo manne yaliyohifadhiwa, ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Korup. Vuguvugu ka kuipinga kampuni ya Herakles Farms lilitoka kwa wananchi, asasi za kitaifa na kimataifa, watafiti, wanasayansi, wanazuoni, na wengine wengi. Hivyo kukawa na shinikizo la juu sana kwa wakati mmoja, yaani kutoka ngazi za chini mahali ambapo kampuni hiyo ilikuwa ikifanya kazi, na pia kukawa na shinikizo la juu toka katika ngazi ya kimataifa, ambako kampuni ilikuwa ikitafuta fedha kwa ajili ya kuanzishia na kugharamia mradi huo. Mwaka 2013, raisi wa Kameruni alisaini mfululizo wa amri ili kupunguza kiwango cha ardhi ambacho mtu au kampuni inaweza kupangishiwa kutoka hekta 73,000 hadi hekta 19,843. Lakini jambo hili bado halikuwapendeza wanajamii wengi na wakawa na nia ya kuendelea kupinga na kusimamia hoja yao ya awali kuwa "Hakuna Mashamba Makubwa Katika Ardhi Yetu". Mwaka 2015

kampuni hiyo iliyatelekeza mashamba yake na shughuli zake katika ardhi za maeneo ya Mundemba na Toko.

Hata hivyo, ushirikiano wa kimataifa kama ule uliohusisha mashirika ya GRAIN/WRM na asasi za kiraia katika ngazi za kitaifa na asasi za wanajamii barani Afrika chini ya usimamizi wa muungano unaohusika katika Kupinga Ukuaji wa Mashamba Makubwa ya Michikichi ya Mawese kwa Matumizi ya Viwanda katika Afrika ya Kati na Magharibi. (*kwa kiingereza: "Alliance Against Industrial Oil Palm Expansion across central and west Africa)*, umefanya kazi ya maana sana ya kuwaamsha wananchi waliokuwa wanateseka kwa kuyafanya mapambano yao yaweze kuonekana, kwa kuwapa taarifa na kisha kwa pamoja kutambua fursa zinazoweza kutumika kuzuia mashamba makubwa ya michikichi ya mawese yanayoleta uharibifu kupitia programu za kijamii za kubadilishana uzoefu na mawazo, kama vile warsha mbalimbali na safari za kuvitembelea vijiji ili kuwatia moyo katika harakati za kupinga uporaji wa ardhi zao. Pamoja na hayo kazi hiyo ya pamoja ililenga kuianika mikakati na mbinu zinazotumiwa na makampuni ya kimataifa yanayopora ardhi za wananchi na kisha kuwatahadharisha wale ambao wapo katika hatari ya kukutana na uporaji huo.

Je, kuna aina nyingine ya mshikamano ambayo ungependa itumike katika kuimarisha upinzani dhidi ya uporaji wa ardhi nchini Kameruni na kwingineko barani Afrika?

Ili vuguvugu la upinzani liweze kufanikiwa, ni muhimu sana kuimarisha mshikamano wa wananchi na kupata safari za mafunzo za kubadilishana uzoefu kati ya vijiji ambavyo vimeathiriwa moja moja na vile ambavyo havijaathiriwa moja kwa moja na miradi mbalimbali ya uwekezaji ili kuwajengea wananchi ujasiri katika ngazi za wananchi. Mambo mengine ya muhimu ni: suala la kubadilishana uzoefu katika ngazi ya mabara ili kushirikishana uzoefu, mambo ambayo yanasaidia sana katika kuuanika uovu wa makampuni na mbinu zao; kuvitembelea vijiji ili kuvitahadharisha vijiji vilivyoathiriwa na ambavyo vinakaribia kuathiriwa juu ya upanuzi mbaya wa mashamba ya michikichi ya mawese na miradi mingine pasipo ridhaa yao; uanikaji imara wa udanganyifu unaofanywa na makampuni kuhusu maendeleo endelevu na jinsi wanavyogubikwa na fedha na makampuni mengine badala ya kuheshimu haki za wananchi kwa kuzingatia Ridhaa Inayozingatia Uhuru, na Taarifa za Awali *(Kwa Kiingereza: Free, Prior and Informed Consent).*

Tunatakiwa kufungamanisha upinzani wa wananchi wa chini pamoja na fursa za jumla za wananchi hao. Tunapaswa kuwekeza katika kujenga uwezo wa asasi za kiraia na wananchi wanaofanya kazi katika ngazi ya chini ili kuwa na "Upinzani wa Wananchi wa Kuaminika" unaoweza kuwaanika na kuwashinda nguvu waporaji wa ardhi na wakiukaji wa haki za binadamu katika bara ambapo kunakuwa na changamoto hizo. Kuandaa mfululizo wa matukio kama vile warsha, semina, safari za kutembelea vijiji, mikutano ya ana kwa ana na ile isiyo ya ana kwa ana na wahusika wakuu.

Kuna hitaji kuu la kujenga ushirikiano imara kati ya jamii na asasi za kaskazini na wenzao wa kusini ili kuweza kushughulikia tatizo la uporaji wa ardhi na uharibifu wa misitu, kwa kuwa mambo hayo yanaletwa na kutekelezwa na wawekezaji pamoja na sera za serikali ikiwemo ile ya chaguo la walaji katika nchi za kaskazini. Mikutano ya kubadilishana uzoefu kati ya wananchi wa Kaskazini na wale wa Kusini itawezesha uwepo wa ufahamu mzuri juu na namna maamuzi ya kisiasa, serikali mbalimbali na makampuni yanavyoleta athari kwa mazingira na ukiukaji wa haki za binadamu Kusini mwa dunia, hasa pale makampuni yanapotoa mawasiliano na matangazo yaliyojaa uongo kwa lengo la kuficha uharibifu na manyanyaso yao, huku wakizitangaza bidhaa zao kuwa ni endelevu.

Kuisimamia haki ya kusema HAPANA: Baraza la Kudumu la Watu wa Afrika ya Kusini

Ph.: Paul Botes.

"Hatutaki uchimbaji wa madini na watu wake. Hatumtaki mtoto wake. Hatumtaki bibi yake. Hatuitaki familia yake. Hatuna hamu wala nia ya kuongea nao au kufanya majadiliano na watu wanaohusika na uchimbaji madini. "

Maneno haya mazito na yenye nguvu yaliongelewa na wawakilishi wawili toka kamati inayoitwa Kamati ya Maafa ya Amadiba *(Amadiba Crisis Committee)* katika kipindi cha Tatu cha Baraza la Kudumu la Watu wa Afrika Kusini kuhusu Makampuni ya Kimataifa kilichofanyika mwezi Novemba 2018. Kamati ya Maafa ya Amadiba inawakilisha jamii ya Xolobeni, jamii ambayo imekuwa ikipambana kwa miaka kumi na sita kuizuia kampuni kubwa ya uchimbaji wa madini ya Australia inayoitwa Transworld Energy and Minerals (TEM), ili isichimbe ardhi yenye utajiri wa madini ya Titanium katika Pwani ya Msituni ya Afrika Kusini. (1) Kwa mujibu wa Kamati ya Maafa ya Amadiba, ardhi ni sehemu muhimu sana ya utambulisho wa jamii kwa wakati uliopita, uliopo, na wakati ujao. Nonhle Mbuthuma, ambaye ni mmoja kati ya waanzilishi wa kundi hilo anasema, "**Tunaamini kwamba tunajitambua kuwa sisi ni akina nani kwa sababu ya ardhi. Tunaamini kuwa mara unapopoteza ardhi, basi unakuwa umeupoteza utambulisho wako.**"

Mwezi Aprili 2018, hiyo Kamati ya Maafa ya Amadiba iliipeleka kesi yao katika Mahakama Kuu ya Afrika Kusini ikiwa ni hatua muhimu sana ya kudai haki. (2) Kwa sasa, yaani baada ya miezi kadhaa kupita, na ikiwa ni wiki chache baada ya kipindi cha Baraza la Watu kupita, **Mahakama zimeamua kwa kuwapendelea wananchi, zikitangaza kuwa Idara ya Rasilimali za Madini ni lazima ipate ridhaa "kamili na rasmi" toka kwa watu wa jamii ya Xolobeni kabla ya kutoa vibali na haki ya kuchimba madini.**

Katika maeneo mbalimbali huko Afrika Kusini na hadi sehemu za mbali, mapambano ya jamii ya Xolobeni yamekuwa ni kesi ya mfano kwa jamii zinazopinga ajenda ya maendeleo inayoburuzwa na sekta ya uziduaji na imeonyesha umuhimu wa mapambano ya kusema HAPANA. Kwa sasa ushindi huu mahsusi umewaamsha na kuwatia motisha wananchi barani Afrika, na ushindi huu umetoa ujumbe na kukumbusha kuwa **haki inawezekana kupitia ujenzi wa vuguvugu la mabadiliko na mshikamano ulioandaliwa vizuri na wenye uendelevu.**

Ni kutokana na moyo huu wa mshikamano na ujasiri madhubuti katika kuzipinga nguvu za makampuni ndio zilizopelekea kuandaliwa kwa kongamano la tatu la Baraza la Kudumu la Watu wa Afrika Kusini kuhusu Makampuni ya Kimataifa. (3) Kongamano hili lilikuwa ni la tatu na la mwisho katika mchakato wa kusikiliza mashauri ambapo wanajamii waliwasilisha kesi

zao dhidi ya makampuni ya kimataifa, huku wakionyesha bayana juu ya ukiukwaji wa haki zao za kibinadamu na haki nyingine; pia walielezea juu ya unyonyaji na uharibifu wa maeneo yao usio na uangalizi maalum. Makampuni haya kwa ushirikiano na Serikali na Mashirika ya Kimataifa ya Fedha kama vile Benki ya Dunia, yamekuwa yakiiendeleza ajenda hii yenye uharibifu ya tasnia ya uziduaji (uchimbaji madini) inayotoa kipaumbele katika kupata faida kuliko watu na sayari yetu—hufanya hayo yote kwa kisingizio cha neno mashuhuri "maendeleo."

"Tumeadhibiwa sana na vitendo vya kikatili vya uziduaji, kuporwa, kuhamishwa makazi na ukatili mwingi unaofanywa na makampuni ya kimataifa katika harakati zao za kutafuta faida," hayo ni maneno yaliyosomwa na Mzee wa Baraza wakati akitoa maelezo ya kufunga siku tatu za baraza hilo. "**Mambo haya yote yamekuwa yakifanywa mara kwa mara kwa njama zinazofanywa na Serikali na watendaji wake na baadhi ya mashirika katika kuwanyamazisha na katika mazingira fulani hata mauaji ya wananchi.** "

Katika kipindi chote cha mchakato wa baraza hilo, wananchi walitoa na kuelezea kesi ishirini dhidi ya Makampuni ya Kimataifa katika nchi za Madagasca, Malawi, Mauritania, Msumbiji, Afrika Kusini, Swaziland, Tanzania, Zambia na Zimbabwe. Kesi hizi zinahusisha makampuni ya uchimbaji madini na ujenzi wa mabwawa makubwa ya umeme, kilimo-biashara kikubwa, na uporaji wa ardhi – na kila kesi mojawapo inaelezea bayana juu ya njama zilizopo kati ya makampuni, serikali na taasisi za kifedha zinazochangia mfumo wa dunia wa ukandamizaji pasipo kuwa na hofu ya kuadhibiwa. (Soma kuhusu hizo kesi hapa)

Mapambano Kuzuia Mabwawa Makubwa ya Umeme: Zuia Inga 3!

Moja kati ya kesi iliyowasilishwa katika Baraza ni ile ambayo wananchi walikuwa wakipinga ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme linalojulikana kama Inga katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). (4) Huku kukiwa na ahadi iliyo nyuma ya mradi huo, yaani "kutoa nguvu za umeme na kufungua ujenzi wa viwanda katika bara la Afrika" huku lengo lao likiwa ni kuifanya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuwa na umeme na pia kutoa umeme kwa bara zima la Afrika. Hadi sasa Mradi wa Mabwawa ya Kuzalishia Umeme wa Inga katika mabwawa yake ya kuzalishia umeme ya Inga 1 na Inga 2 yameshawafanya wananchi wengi wa DRC kuwa hawana makazi. Ikiwa ujenzi wa bwawa la kuzalishia umeme la Inga 3 utaendelea kama ulivyopangwa, basi ni dhahiri kuwa takribani watu 37,000 au zaidi watakabiliana na adha ya kupoteza makazi na njia zao nyingine za kujikimu kimaisha.

Makampuni ya uchimbaji wa madini yamepata faida sana kutokana na umeme unaozalishwa toka katika mabwawa mawili ya kuzalishia umeme ya Inga, huku wananchi wengi wakiwa hawana umeme wa uhakika. Kwa sasa, asilimia 85% ya wananchi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) hawana umeme. (5) Mpango uliozinduliwa hivi karibuni unaojulikana kama Mpango Fungamanishi wa Rasilimali wa Afrika Kusini *(Kwa Kiingereza: South Africa's Integrated Resource Plan)* unaendeleza makubalino kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Afrika ya Kusini ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme kufikia kiasi cha megawati 2500MW za umeme ifikapo mwaka 2030. (6) Kwa sasa, **watu wanaoathirika moja kwa moja kutokana na mradi huu mkubwa hawatapata faida yoyote ile huku umeme ukipelekwa katika nchi sita ili kuwezesha uchimbaji wa madini na shughuli nyingine za tasnia ya uziduaji nchini Afrika Kusini.** "Sisi tunalala katika maeneo yaliyo na mradi wa mabwawa ya umeme wa Inga lakini tunaishi gizani," maneno hayo yalisemwa na Jane*, ambaye ni mwanamke mwanaharakati kiongozi wa Kikongo aliyeongea wakati wa Baraza la Watu.

Wakati wa Baraza hilo, wanaharakati walisisitiza pia juu ya mzigo ambao wanawake wanaubeba mara kunapokuwepo na miradi mikubwa kama huu wa Inga ambao unatishia maisha ya watu na shughuli zao za kujikimu kimaisha. Mwanamke mmoja mwanaharakati alisema hivi: "Sisi tunategemea kilimo – tutawezaje kupata chakula chetu? Tutafanyaje ili

tuweze kuwalisha watoto wetu? Tutaishije kwa ujumla? Sisi, wanawake tunaoishi Inga tunakitegemea sana kilimo – ni kilimo ndicho kinachotuwezesha kuwalisha watoto wetu. Kwa sasa tunaona hali ya ukavu tu kwa sababu ya bwawa lililojengwa. Uwezo wetu wa kuzalisha chakula umepungua sana kwa sababu ya uwepo wa miundo mbinu mingi inayohusiana na hili bwawa. Kuna wakati ili mlazimu mume wangu kusafiri hadi kijiji kingine ili aweze kuwinda mnyama mdogo kwa sababu kijijini kwetu wanyama wameanza kutoweka. Sisi, tunaoishi karibu kabisa na bwawa la umeme hatuna hata huo umeme."

Wananchi wanaopambana na bwawa la Inga 3 wameshawasiliana na Serikali zinazohusika, na wameandika barua kwenda kwa serikali ya Afrika Kusini. Pia wamezindua kampeni ya *Kupinga na Kuzuia Inga 3 (saini tamko la kuwaunga mkono na kuonyesha mshikamano)*. Wananchi wanadai na wanataka kampuni zinazojihusisha na ujenzi huo za Kichina, Kihispania, na Afrika ya Kusini ziondoke na ziachane na mpango huo; pia wanaitaka Serikali yoyote ile isishiriki katika uendelezaji wa mradi huo. **Upinzaji wao unatoa hamasa sana. Wanafanya kazi katika mazingira ya kutishwa sana ilhali wakiendelea kupambana kuidai na kuipata haki yao ya Kusema HAPANA na kuendelea kudai fidia kwa wale ambao walipoteza makazi yao kutokana mabwawa ya umeme ya Inga 1 na 2.**

Wananchi kutoka Afrika Kusini wameshaanza kushughulikia madai ya wanajamii wa Inga, wanaona ndio fursa ya wazi kabisa ya kuwa na mkakati wa pamoja na mshikamano ili kuiwajibisha serikali ya Afrika ya Kusini. "Mto Kongo ni mali ya watu lakini watu wameshaporwa mto huo. Wananchi hawakuwahi kushirikishwa wala kuombwa ridhaa yao. Sisi tuliopo hapa Afrika Kusini hatukuwahi kuelezwa kuwa tutapata umeme toka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Na hata kama tungepata umeme toka huko, ni hakika tusingeufurahia umeme huo hasa baada ya kuyafahamu maasi, ubabe wa kivita, na uharibifu unaofanyika katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo," kauli hiyo ilitolewa na Caroline Ntaopane toka muungano unaojulikana kama Mtandao wa Afrika wa Wanawake Dhidi ya Uziduaji wenye Uharibifu *(Kwa Kiingereza: African Women network against destructive resource extraction -WoMin Alliance).*

Baraza la Watu limekuwa ni jukwaa muhimu sana kwa wananchi wa maeneo ya Kusini mwa Afrika kuweza kushirikishana mapambano yao na kujenga mshikamano, kuwasilisha kesi nzito zinazohusu ukiukwaji wa makampuni, na kutoa changamoto kwa mazoea yanayohusisha neno "maendeleo" kwa kuuanika ukatili ulio ndani yake na hali isiyo endelevu. "

Kwa sasa wananchi hao na wengine wengi, wanafanya kazi kwa pamoja kujenga kampeni inayotoa fursa na *Haki ya Kusema Hapana*. Kampeni hii ni "uhamasishaji mpana na makutano ya uanaharakati wa kimataifa na mshikamano." Kampeni hii ina msingi wake katika kanuni inayozingatia Uhuru, na Taarifa za Mapema kabla ya Kutoa Ridhaa *(Kwa Kiingereza: Free, Prior and Informed Consent - FPIC*) na kampeni hii inajengwa katika nguvu ya kuandaa mavuguvugu ya mabadiliko, umoja, mashirika ya wanawake na mashirika mengine mengi yaliyo katika jamii kama vile ilivyokuwa kwa jamii ya Xolobeni huko Afrika Kusini na huko Inga katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), yaani makundi yote yanayoinuka na kusema HAPANA kwa nguvu za makampuni, njama za serikali, na kwa ajenda ya maendeleo yenye uharibifu inayowaathiri watu na sayari yetu.

Maggie Mapondera
WoMin African Alliance, http://www.womin.org.za/

** Jina la kiongozi mwanaharakati lilibadilishwa kwa sababu za kiusalama*

(1) CIDSE, Xolobeni Community and the Struggle for Consent, November 2017, https://www.cidse.org/gender-equality-blog/xolobeni-community-and-the-struggle-for-consent.html
(2) The Guardian, South African community wins court battle over mining rights, November 2018, https://www.theguardian.com/environment/2018/nov/22/south-african-community-wins-court-battle-

over-mining-rights
(3) https://www.stopcorporateimpunity.org/permanent-peoples-tribunal-transnational-southern-africa/
(4) Daily Maverick, SA does not need the Grand Inga Project, November 2018, https://www.dailymaverick.co.za/opinionista/2018-11-08-sa-does-not-need-the-grand-inga-project/
(5) No to Inga 3, Yes to accessible energy across Congo, https://stopinga3.org/en/
(6) South African government releases Integrated Resource Plan draft, August 2018, https://africaoilandpower.com/2018/08/28/south-african-government-releases-integrated-resource-plan-draft/

Tanzania: Upinzani wa wanajamii dhidi ya mashamba makubwa ya miti

Kwa mtazamo wa mara ya kwanza, kijiji cha Nzivi kinafanana na vijiji vingine katika eneo lile. Lakini kijiji hicho kina tofauti kubwa na vijiji vingine kwa sababu hakiruhusu wawekezaji wanaotaka kupanda mashamba makubwa kama vile upandaji wa mashamba makubwa ya miti. Kampuni ya Green Resources ni kampuni kubwa zaidi inayojihusisha na upandaji wa mashamba ya miti nchini Tanzania. **.**

Kwa mtazamo wa mara ya kwanza, kijiji cha Nzivi, kilichopo katika mkoa wa Iringa nchini Tanzania, kinafanana sana na vijiji vingine vingi katika eneo lile. Wakazi wake wanaishi kwa kutegemea shughuli za kilimo na ufugaji wa ng'ombe, na hizo ndizo kazi kuu wanazozifanya wananchi wa kijiji hiki. Lakini mtu yeyote atakaye kitembelea kijiji hiki atashangazwa na mashamba makubwa ya miti yaliyokizunguka kijiji hicho, mashamba hayo makubwa ya miti ni yale ya miti ya paina na mikaratusi. Kwa ujumla wake, inawezekana ikawa ndio mashamba makubwa zaidi ya miti katika nchi za Afrika ya Mashariki. Hadi kufikia mwaka 2016, Tanzania ilikuwa na takribani hekta laki 583 zilizokuwa zimepandwa miti, kati ya hizo hekta zaidi ya laki 400, ambazo ni wastani wa asilimia 70 zinapatikana katika mikoa ya Iringa na Njombe, eneo linalojulikana kama Nyanda za Juu Kusini.

Lakini mtu yeyote atakaye zungumza na wanajamii wa kijiji cha Nzivi atagundua kuwa wananchi wa kijiji hicho wapo tofauti ukilinganisha na vijiji vingine kwa kuzingatia mambo makuu mawili: baada ya kuwa wamejifunza kutokana na uzoefu wa vijiji vingine, waliamua kutoruhusu wawekezaji wakubwa ikiwemo uwekezaji wa mashamba makubwa ya miti. Na kutokana na uamuzi huo, kijiji cha Nzivi bado kina eneo kubwa la ardhi linalotumika kwa mahitaji ya msingi ya wanakijiji wote.

Ili kufahamu sababu zilizowafanya wanakijiji wa Nzivi kufanya maamuzi hayo, ni vema kufahamu athari za mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda kwa jamii zingine katika eneo lile. Mwaka 2018, mashirika ya kiraia ya SUHODE Foundation, Justiça Ambiental na WRM yalitembelea vijiji mbalimbali. Pamoja na kukitembelea kijjiji cha Nzivi, yalitembelea pia vijiji vya Idete, Mapanda, Kihanga, Igowole na Taweta, vijiji ambavyo pia vinakabiliana na mashamba makubwa ya miti yanayomilikiwa na kampuni ya Green Resources. Lengo la

safari hii ilikuwa ni kujifunza juu ya athari zinazoletwa na uwepo wa mashamba makubwa ya miti katika maeneo hayo.

Kampuni ya Green Resources nchini Tanzania

Mashamba makubwa ya miti yaliaanza kupandwa katika maeneo hayo miongo kadhaa iliyopita, kwa mara ya kwanza mashamba hayo yalianzishwa na kampuni ya serikali iitwayo Sao Hill, na baadaye kuanzia miaka ya 1990, mashamba makubwa ya miti yalianza kuongezeka kupitia makampuni binafsi. Kampuni kubwa binafsi inayofanya kazi za upandaji wa mashamba makubwa ya miti ni kampuni ya Green Resources, ambayo ni kampuni ya Kinorway, inayomilikiwa kwa sehemu kubwa na taasisi ya serikali ya Norway inayoshughulikia masuala ya maendeleo inayoitwa Norfund. Pia kuna wawekezaji wakubwa wenye hisa zao katika kampuni hiyo. (1)

Kampuni ya Green Resources inajieleza kuwa ndio kampuni kubwa inayoendeleza 'misitu' na inayochakata mbao na bidhaa zake katika Afrika ya Mashariki, huku ikiwa na mashamba makubwa ya miti huko Msumbiji, Uganda, na Tanzania. Nchini Tanzania kampuni ya Green Resources inamiliki eneo lenye ukubwa wa hekta 74,850 ambapo kati ya hizo hekta 17,000 zikiwa zimeshapandwa tayari miti aina ya mikaratusi na paina. Kampuni hii inakiri katika tovuti yake kuwa "inaamini upandaji wa miti ni moja kati ya njia makini zaidi ya kuboresha hali za kijamii na kiuchumi kwa watu waishio vijijini na kwamba kampuni inalenga kuwa ndio mwajiri na mshirika anayependwa zaidi na wanajamii katika maeneo hayo." Pia kampuni hii inaeleza kuwa kwa upande wa Tanzania "Eneo lililotumika kwa upandaji wa miti ni eneo lenye thamani ndogo na lenye nyasi tupu na ambalo limepatikana toka kwenye vijiji."

Kinyume na ilivyo huko Msumbiji ambapo kwa sasa kampuni hii imepoteza hati yake (cheti), huko Tanzania, kampuni hii imepata hati toka FSC (Forest Stewardship Council), hati ambayo inairuhusu kampuni hii kudai kuwa mbao zake au mazao yake mengine ya miti yanatoka katika vyanzo 'endelevu.' Pia kampuni hii imeyasajili na kuyathibitisha mashamba yake ya miti kwa ajili ya utunzaji wa hewa ukaa (kupitia mfumo unaojulikana kwa kifupi kama VCS), na pia mashamba hayo pia yapo chini ya utaratibu ujulikanao kama CCBS, ambao pamoja na mambo mengine, kampuni inadai kuwa "utume wake" ni " kuhamasisha na kukuza shughuli za usimamizi bora wa ardhi ambazo kwa hakika zinapunguza mabadiliko ya tabia-chini duniani, na kwamba zinaboresha maisha na kupunguza umaskini kwa jamii za vijijini huku zikihifadhi bayo-anuai." (2)

Kampuni ya Green Resources iliwasili kwa wanajamii ya Idete mwaka 1996, Mapanda mwaka 1997 na Taweta mwaka 2007. Wanajamii walilaghaiwa kisha wakakubali kuingia mkataba wa makubaliano na kampuni ambayo ilifanikiwa hatimaye kuchukua eneo kubwa sana kiasi cha theluthi ya ardhi ya wananchi kwa kipindi cha miaka 99. Jambo hili lilitokea kutokana na sababu kuu mbili. Kwanza, wakati huo wananchi hawakufahamu umuhimu wa maeneo ya ardhi yaliyotolewa ama kukodishwa kuwa yana umuhimu sana kwao na wala walikuwa hawafahamu thamani halisi ya maeneo hayo. Lakini sababu nyingine kuu iliyowafanya kuikubali na kuipokea kampuni ya Green Resources ni orodha ya ahadi nyingi zilizotolewa na kampuni ya Green Resources. Kwa kuanzia, moja kati ya ahadi hizo ni ajira, pamoja na maboresho mengine ya miundo-mbinu ya vijiji; kama vile kujenga na kukarabati madarasa, kumbi na ofisi za serikali za vijiji, zahanati, vyanzo vya maji, pamoja na makazi ya wafanyakazi wa afya na walimu. Pamoja na ahadi hizo pia kampuni iliahidi kuwapatia asilimia 10 ya mapato yatokanayo na mauzo ya hewa-ukaa ambayo kimsingi yanatokana na kiasi cha hewa ukaa 'kilichohifadhiwa' katika misitu ya paina na mikaratusi iliyopandwa na kukua vizuri katika vijiji hivyo vitatu. Kampuni ya Green Resources iliweka ahadi hizi kwa maandishi na kisha ikasaini mikataba ya nyongeza na wanajamii kwa ajili ya malipo yatokanayo na mauzo ya hewa ukaa huku wananchi wakiwa hawafahamu sawasawa jinsi mfumo wa masoko ya hewa ukaa unavyofanya kazi.

Kwa sasa, baada ya kuwa kampuni hii imewasili miaka mingi iliyopita, wananchi wamekatishwa tamaa na wana hasira. Wananchi wanakiri kuwa ahadi nyingi za kampuni ya Green Resources hazijatekelezwa na badala yake ni ahadi chache tu zilizotekelezwa. Kwa sasa, hakuna ajira zozote zile za kudumu zilizotengenezwa. Katika vijiji vya Idete na Taweta, kampuni ya Green Resources imetengeneza ajira moja tu ya kudumu, na katika kijiji cha Mapanda ambacho kwa mujibu wa serikali ya kijiji kina idadi ya wakazi 5,503 – hakuna hata ajira moja ya kudumu. Pia wanavijiji wana malalamiko mengi sana kuhusiana na mazingira ya kufanyia kazi, ikiwemo mishahara midogo, ukosefu wa usafiri kwa wale walioajiriwa kwa ajira za muda mfupi; ikiwemo ukosefu wa vifaa maalumu vya kujikinga dhidi ya sumu zilizo katika pembejeo za kilimo. Pa wanavijiji wanailaumu kampuni ya Green Resources kwa kutowasilisha/kulipa michango yao ya mafao kwa mamlaka husika huku wao wakiwa wamekatwa hizo fedha toka katika mishahara yao kwa ajili ya kuchangia katika mifuko hiyo ya mafao ya kijamii.

Wanavijiji wanakiri kuwa baadhi ya miundo mbinu iliyo ahidiwa imetekelezwa. Lakini wakati huo huo katika kijiji cha Mapanda, bado wanakijiji wanangojea ukumbi wa mikutano na ofisi mpya kama ilivyoahidiwa na kampuni. Hatimaye kampuni ya Green Resources imeahidi kujenga ukumbi huo mpya mwaka huu baada ya kuwa imepata shinikizo la kutosha toka kwa wanajamii. Hata hivyo, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2018 ukumbi huo ulikuwa bado haujajengwa wala kukamilika. Katika kijiji cha Taweta, jambo pekee ambalo wanakijiji wanalikumbuka ni ukarabati wa vyumba viwili vya madarasa. Ofisi ambayo ilijengwa na kampuni ya Green Resources katika kijiji hiki kwa ajili ya kusimamia mashamba makubwa ya miti katika eneo hilo imefungwa na inaonekana kuwa imetelekezwa.

Mauzo ya hewa ukaa yalitolewa gawio kwa kijiji cha Mapanda peke yake, ambapo wananchi walipokea malipo ya hewa ukaa kwa kiasi cha fedha za Tanzania milioni 30 na millioni 33, malipo hayo yalifanyika mwaka 2011 na mwaka 2014. Malipo hayo yaliyofanyika kwa ujumla wake yanafikia kiasi cha dola za kimarekani elfu 40, kiasi ambacho ni kidogo sana kwa kijiji chenye watu zaidi ya elfu 5 huku kikiwa na changamoto kubwa ya miundo mbinu kama vile uhitaji wa kuboresha mfumo wake wa maji safi. Pamoja na hayo, hakukuwa na uwazi kuhusiana na namna kiwango hicho cha fedha kilicholipwa kwa wanajamii kilivyopatikana. Wananchi walikuwa hawafahamu thamani halisi ya mauzo ambayo kampuni imepata kutokana mauzo ya hewa ukaa iliyohifadhiwa katika eneo lao, pia walikuwa hawafahamu ikiwa fedha walizolipwa ni asilimia 10 au la ya mauzo ya hewa ukaa ambayo kampuni ilikuwa imepata. Vijiji vya Idete na Taweta havijapokea malipo yoyote yale kutokana na mauzo ya hewa ukaa hadi sasa. Katika mada iliyowasilishwa na kampuni ya Green Resources kwa ajili ya watu wote inayopatikana katika mtandao wa intaneti (3), kampuni inalalamika kuwa "malipo ya hewa ukaa yanakatisha tamaa", lakini kampuni inaeleza kuwa hata hivyo kampuni ya "Green Resources imezalisha au kupata dola za kimarekani millioni 2 (…)". Ikiwa mtu atapiga hesabu ya asilimia 10 ya kiasi hicho cha fedha, basi ni dhahiri kuwa wanakijiji walipaswa kupokea walau dola za kimarekani laki 200 – kiasi ambacho ni kikubwa zaidi kuliko kiasi ambacho wanakijiji wa Mapanda walilipwa.

Wanajamii katika vijiji vitatu tulivyovitembelea wanajuta kutoa ardhi yao kubwa kwa kampuni hii na kwamba kwa sasa wanazuiwa kuingia katika ardhi hiyo hata kwa shughuli ya kukusanya au kukata nyasi au kuchimba udongo wa mfinyanzi katika maeneo ambayo bado hata hayajapandwa miti. Walipoulizwa ikiwa wanakubaliana na madai ya kampuni kuwa ardhi waliyotoa ina 'thamani ndogo' na kwamba ilikuwa 'imeharibiwa' (kama ambavyo kampuni ya Green Resources na makampuni mengine ya upandaji miti wanavyodai), wananchi walijibu kwa pamoja kuwa madai hayo ni uongo mkubwa. Wananchi wanafahamu kuwa ardhi hiyo ni ya thamani sana, yenye rutuba, na ambayo ni muhimu kwao na hatma yao ya baadaye. Kwa sasa ikiwa wanataka kuingia katika ardhi hiyo ni lazima waombe kibali cha kufanya hivyo. Katika kijiji cha Idete, wananchi wanahofia kuwa wanashindwa kukusanya au kuvuna aina fulani ya magugu yanayojulikana kwa lugha ya kienyeji kama (*Milulu*) yanayotumika kutengenezea vikapu vya asili ambavyo hutengenezwa zaidi na wanawake. Pia mwanakijiji

mmoja mwanamke anahofia juu ya ongezeko la maambukizi ya VVU/UKIMWI kutokana na ongezeko la wafanyakazi toka nje ya maeneo ya kijiji cha Idete.

Mwanakijiji mwingine anadai kuwa hakuna namna ya kuweza kulinganisha manufaa waliyoyapata hadi sasa dhidi ya hasara na taabu ambazo wananchi wanazipata baada ya kuitoa na kuikodisha ardhi yao kwa miaka 99. Kwa hakika wanakijiji walio wengi wanahofia sana maisha yao ya baadaye. Mwanamke mmoja wa kijiji cha Idete alitafakari kwa kina na kwa huzuni juu ya hatma ya watoto wake ikiwa watapata ardhi ya kulima hapo baadaye, na alisema kwa hali ilivyo ana hakika kuwa wajukuu zake watakosa eneo la kuzalisha mazao ya chakula na kufugia mifugo na kwamba kwa sababu hiyo umaskini utaongezeka sana.

Sio jambo la kushangaza, kwa sasa wananchi katika vijiji vitatu wanataka ardhi yao inayomilikiwa na kampuni ya Green Resources irudishwe kwao au angalau sehemu ya ardhi irudi mikononi mwao. Huku wakitafakari juu ya hatma yao ya baadaye, wananchi wengi katika vijiji hivyo wanataka kuwa na uhakika kuwa watakuwa na ardhi ya kutosha kwa idadi kubwa ya wanavijiji katika jamii zao, yaani miaka michache ijayo. Hivyo hivyo wanavijiji hao wanakabiliana na changamoto kubwa kwa kuwa wamesaini mikataba ya kisheria ambapo wamekubali kukodisha ardhi zao za vijiji kwa kampuni hiyo ya Green Resources. Lakini, mikataba hiyo ina uhalali gani ilhali ilikubaliwa kwa msingi wa orodha ya ahadi nyingi ambazo hazijatekelezwa huku shughuli za kampuni hiyo zikiendelea kuweka hatma ya baadaye ya wananchi hao mashakani?

Mambo yaliyogunduliwa katika safari ya kutembelea vijiji hivyo yanatoa msingi wa kutoa hoja ili kuhoji ukweli wa maelezo ya kampuni pale inaposema kuwa nchini Tanzania kampuni inafanya kazi vizuri na kwamba ni mshirika anayependwa zaidi na wanajamii wa maeneo ya vijijini.

Taarifa ni Nguvu

Habari hizi kuhusu kampuni ya Green Resources nchini Tanzania inaonyesha kuwa makampuni ya upandaji miti wanachohitaji wakati wote ni kupata ardhi kubwa ili waweze kufanya shughuli zao. Pia inaonyesha jinsi ambavyo makampuni haya yanafanya hivyo kwa msingi wa kutoa ahadi za uongo au ahadi zinazotekelezwa vibaya kwa nia tu ya kuwashawishi wananchi ambao hatimaye huathirika kwa kuikodisha ardhi yao. Maelezo na uzoefu toka kwa jamii zinazokabiliana na kampuni ya Green Resources na makampuni mengine ya mashamba ya miti ni muhimu sana kwa vijiji vingine ili viweze kujifunza na kutafakari vizuri.

Wanakijiji wa Nzivi waliweza kuyafahamu haya kwa wakati na walipata uzoefu toka katika vijiji vingine hasa walipokuwa wakiongea na vijiji jirani, na wakawa na mashaka kuwa na wao wasije wakakutana na hali kama hiyo ya kusikitisha, na kwa msingi huo waliamua kutoziamini ahadi za makampuni na wakaamua kusema *hapana* kwa kampuni yoyote ile inayotaka kupata kiwango kikubwa cha ardhi yao kama vile Green Resources. Waliamua kubakia na usimamizi na uthibiti wa ardhi yao kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Hii haimaanishi kuwa wanakijiji wa Nzivi hawawezi kupokea uwekezaji wowote ule. Viongozi wa kijiji walitueleza kuwa wametenga eneo dogo la ardhi ya kijiji kwa ajili ya wawekezaji, na kwamba eneo hilo ni maalum kwa wawekezaji wasiohitaji eneo kubwa la ardhi yao na walio tayari kusaidia na kuunga mkono huduma za kijamii ambazo ni muhimu na hazipo kama vile elimu na afya. Wananchi wanaamini kuwa aina hiyo ya uwekezaji usiohitaji ardhi kubwa na unaounga mkono huduma za kijamii ni wa muhimu sana maana utaendelea kulinda haki ya kumiliki ardhi yao, misitu, na mbuga zenye nyasi vitu ambavyo wanavitegemea katika maisha yao ya kila siku.

Jambo la ajabu, hakuna mwekezaji aliyeonekana kutoa ombi kwa wananchi wa kijiji hicho. Hii inaonyesha jinsi wawekezaji waliogubikwa na nia ya kupata faida kama vile kampuni ya Green Resources na wadau wake wasivyokuwa na nia ya kusaidia mahitaji ya watu wa vijijini nchini Tanzania kama ilivyo kwa kijiji cha Nzivi.

Justiça Ambiental! - Mozambique, SUHODE Foundation - Tanzania na WRM

(1) http://www.suaire.suanet.ac.tz:8080/xmlui/bitstream/handle/123456789/1659/SAID%20ASIAD.pdf?sequence=1&isAllowed=y
(2) http://www.greenresources.no and http://www.climate-standards.org/about-ccba/
(3) http://www.greenresources.no/Portals/0/pdf/GR_NewForest_for_Africa_170316_(new).compressed.pdf

Makala za Taarifa Hii Rasmi ya Habari zinaweza kuchapishwa na kutawanywa kwa kupitia chanzo hiki: **Bulletin 241 of the World Rainforest Movement (WRM): "Voices from the Ground: Communities in Movement and Resistance Strategies"** (https://wrm.org.uy/)

*Taarifa Rasmi ya Habari ya WRM imedhamiriwa kuwa ni **nyenzo ya kusaidia na kuunga mkono mapambano ya wanajamii wanaolinda ardhi na misitu yao.** Pia taarifa hii imedhamiriwa **kuzifanya sauti za mapambano mengi ya upinzani kusikika na kufahamika**, Hivyo, katika kila toleo, tunajaribu kuwaalika watu na makundi tofauti kuchangia makala zao au kutoa taarifa zao nyingine ambazo ni muhimu. Zaidi ya yote, taarifa hii inalenga kuwa ni **nyenzo ya kuwafahamisha** watu wanaotegemea misitu kuhusu mipango na juhudi za kimataifa zinazohusu misitu **na kuwaonya** juu ya uwezekano wa hatari na athari zinazoweza kuwakuta katika maisha yao.*

Taarifa rasmi ya habari ya WRM inatawanywa kwa barua-pepe, na kupitia mitandao ya kijamii kama vile Facebook na twitter na pia unaweza kuisoma taarifa hii katika tovuti ya WRM. Kama hadi sasa hupokei taarifa hii, unaweza kujiunga na kupata taarifa hii bure katika tovuti ya WRM (http://wrm.org.uy). Ikiwa utapenda kuchangia wazo au makala au ikiwa utapenda kuangazia mapambano katika ngazi ya kimataifa, basi tunaomba uandike barua pepe kwenda wrm@wrm.org.uy